SUPA JACKPOT
TZS. 1,074,741,067
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**NSSF yalipa bilioni 2.6/- vyeti feki**

UKURASA 3




UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Februari 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581216
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# PSSSF TAABANI

• **Bunge** labaini uwezo kulipa mafao mdogo, serikali yaagizwa... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wazazi wa wanafunzi 140 wa Shule ya Sekondari ya Thaqafa, Nyamagana mkoani Mwanza, wakiwa wamekusanyika nje ya shule hiyo jana, wakitaka kujua hatima ya watoto wao waliofutiwa matokeo ya mitihani ya kidato cha nne kutokana na udanganyifu unaodaiwa kufanywa na shule. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Wabunge waja juu ubadhirifu mabilioni fedha za halmashauri

UKURASA 3

## Watu 12 mbaroni tuhuma za wizi mitihani kidato cha IV

UKURASA 2



REACH A WIDER AUDIENCE THIS Valentine SEASON
AT AN AMAZING OFFER UP TO 25% Off
On valentine season advertisements*
FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023
The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY
Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY
TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com
*Terms and conditions apply.
Followus: @Theguardiantz




Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Daniel Charles Pancras (kulia), akizungumza katika mkutano wa siku mbili wa wadau wa sekta ya ufugaji nyuki, jijini Dar es Salaam jana. Mkutano huo, umelenga kuwaelimisha wadau hao kuhusu njia thabiti za kuongeza ubora wa usindikaji na uuzaji wa bidhaa za nyuki, ili kuongeza ushindani kwenye soko la ndani na la kimataifa. **PICHA: CARLOS BANDA**

# PSSSF taabani kisa ulegevu michango

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilibaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) uko taabani kifedha kutokana na waajiri kutokuwasilisha michango ya wanachama, hivyo kushindwa kuwalipa mafao wastaafu kwa wakati.

Kutokana na hali hiyo, kamati hiyo imeliomba Bunge kuishauri serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria waajiri ambao hajawasilisha michango kwa wakati na ukamilifu kwenye mfuko huo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Joseph Mhagama, alisema hayo bungeni jijini jana wakati akisoma taarifa ya mwaka ya shughuli ilizofanya.

"Kamati inaomba Bunge lishauri serikali PSSSF ifuatilie michango na kulipa kikamilifu. Itoe elimu ya mara kwa mara kwa wanachama kuhusu umuhimu wa kufuatilia na kupata taarifa zao binafsi na michango yao," alisema.

Kuhusu hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, alisema kwa kuwa zina mchango mkubwa kiuchumi, serikali iongeze jitihada za kuhamasisha watu wengi zaidi kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kuweka mfumo na njia rahisi kwa watu kufanya hivyo.

**MAAZIMIO KUTOTEKELEZWA**

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Dk. Jasson Rwekiza, alisema uchambuzi wa kamati umebaini kutotekelezwa kwa sehemu ya maazimio ya Bunge na baadhi ya wizara zimeandaa marekebisho ya sheria ndogo ambayo yamefikia hatua mbalimbali pasipo kuzingatia maazimio yaliyotolewa.

Alisema hatua ya kutokamilika kwa rasimu ya marekebisho baadhi ya wizara zilizobainika kuwa katika hatua hiyo ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kuhusu ucheleweshaji wa maazimio ya kurekebisha sheria ndogo, Bunge limeazimia kwamba mamlaka zilizobainika kuchelewa zikamilishe mchakato wa marekebisho ndani ya siku 20 kuanzia jana (Februari 8).

Pia alisema suala la kutokutekelezwa kwa maazimio, mamlaka husika zitekeleze ndani ya siku 30 kuanzia jana.

"Kuhusu kukinzana na masharti ya katiba, Bunge limeazimia, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba zifanye marekebisho ndani ya siku 60.

"Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kufungwa kwa sheria ndogo na sheria nyingine za nchi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizozitunga zirekebishe ndani ya siku 60 ili kuondoa dosari hiyo," alisema.

Katika suala la kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, alisema Bunge limeazimia mamlaka husika zirekebishe dosari hiyo ndani ya siku 60.

Pia kuhusu masharti yasiyo na uhalisia alisema Bunge limeazimia mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia zifanye marekebisho ndani ya siku 60 na dosari ya uandishi wa majedwari zirekebishwe ndani ya siku 60.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kigoma, Sylvia Sigula, alisema changamoto ya sheria ndogo ni kubwa kwa kuwa zinakosa uhalisia, hazitekelezeki na kuleta matatizo kwa wananchi.

"Ukiangalia sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya wilaya ya Misungwi ya mwaka 2022, inatoa katazo la watu kufanya shughuli yoyote ya maendeleo kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa nne asubuhi kwa lengo la kufanya usafi, tuondoe hili zuio la kusema shughuli za maendeleo zozote zisifanyike kwa saa hizi, na utekelezaji wake haiwezekani," alisema.

Alisema kuna haja ya serikali kuleta sheria hiyo bungeni ili ifanyiwe marekebisho.

Alisema kuruhusu sheria hizo zianze kutumika kabla hazijapitiwa na Bunge kimekuwa kichaka cha wananchi kuteswa na sheria, kanuni mbovu na zinapofikishwa bungeni tayari watu wameshaumia.

"Nina ombi kuna haja kama Bunge kufanyia marekebisho kifungu cha 37 cha sheria ya tafsiri, kuondoa hali ya kuruhusu sheria kuanza kutumika kabla hazijapitiwa na Bunge.

Pia alisema haiwezekani abiria atupe takataka kwenye basi halafu faini ilipwe na mwenye basi na kwamba kamati imeshauri kama kosa litafanywa na abiria awajibishwe vivyo hivyo kwa konda au mmiliki wawajibishwe waliotenda kosa.

"Mwaka 2019 Bunge tulipitisha sheria ndogo ni kanuni ya kukataza mifuko ya plastiki na leo ni miaka mitatu, Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nikupe taarifa mifuko ya plastiki ipo mitaani, inatumika na serikali ipo kimya haitoi tamko lolote kuhusu kinachoendelea, bunge tunakaa hapa tunapitisha sheria na kutoa maazimio lakini utekelezaji unakuwa na changamoto hizo," alisema.

# Mbaroni madai wizi mitihani kidato cha nne

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema watu 12 hadi sasa wako mahabusu wakihusishwa na madai ya wizi wa mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2022.

Pia amesema uchunguzi bado unaendelea kwenye vituo vilivyobainika kufanya udanganyifu wa mitihani huku watumishi waliosimamia mitihani hiyo barua zao zikiandikwa kwa mamlaka zao za ajira ili kuchukuliwa hatua na kushtakiwa.

Prof. Mkenda alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu wazazi wa wanafunzi 140 waliofanya mtihani huo katika Shule ya Sekondari ya Thaqaafa, jijini Mwanza, walioandamana kushinikiza viongozi wa juu wa serikali kuingilia kati suala hilo ili kupata matokeo ya watoto wao.

Alisema serikali imeridhishwa na uamuzi uliofanywa na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) kuhusu wanafunzi 337 waliobainika kufanya udanganyifu kwenye mitihani hiyo.

"Sisi na uongozi wa baraza tumekutana na kila kundi la wale ambao matokeo yao yamefutwa. Tumejiridhisha na tungependa kutoa matokeo yafuatayo, wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne ni 560,335 kati ya hao wanafunzi waliofutiwa matokeo ni 337.

"Hii ni asilimia 0.06 ya watahiniwa wote ni asilimia ndogo sana lakini inagusa Watanzania wenzetu. Wanafunzi wengine 20 matokeo yao hayajafutwa, yamezuiwa bado uchunguzi unaendelea na utakapokamilika, baraza litachukua hatua stahiki," alisema.

Prof. Mkenda alisema kati ya wanafunzi waliofutiwa matokeo wanafunzi wanne waliandika matusi, wako wanafunzi 51 waliokutwa na maandishi yasiyoruhusiwa kwenye chumba cha mtihani, wanafunzi 10 walikamatwa na simu au 'smart watch' na watahiniwa tisa wenyewe kufanya mitihani.

"Wanafunzi 27 walikamatwa wakisaidiana kwenye chumba cha mtihani. Wako sita kwa sababu ya kutumia jukwaa la 'whatsapp' kusaidiana kwenye mitihani hii imetokea kwenye shule ya Mnemonic Academy ya Zanzibar," alisema.

Pia alisema watahiniwa 20 waliofanya mtihani pale matokeo yao yamezuiwa hayajafutwa kwa sababu kuna majina 20 kwenye kundi la 'whatsapp' hayalingani na waliofanya mtihani, hivyo haijulikani ni kina nani kwa hiyo uchunguzi unaendelea.

"Wanafunzi 206 wamefutiwa matokeo kwa sababu ya kufanana kwa majibu waliyotoa kwenye mitihani yao. Kati yao, 140 wanatoka kwenye shule na kituo cha Thaqaafa jijini Mwanza ambacho wazazi walikuwa wanaandamana na watahiniwa 66 wanatoka Twibhoki mkoani Mara," alisema.

Mkenda alifafanua kuwa taarifa za siri ziliwasilishwa kwenye baraza kuhusu wizi kwenye vituo hivyo na baraza likachukua hatua ikiwamo kupitia majibu yaliyoandikwa na wanafunzi.

"Kwenye kusahihisha walipopata walipata wote lakini walipokosa walikosea wote kwa namna moja, lazima watu wamewekwa mahali na kufundishwa. Kwenye darasa la saba, matokeo yalifutwa kwa namna hii hii na baraza liliwaruhusu kurudia mtihani waliporudia kulikuwa hakuna kufanana kwa majibu," alisema.

Alisema kwenye shule ya Thaqaafa watahiniwa walikuwa 192 lakini watahiniwa ambao majibu yamefanana ni 140 ambao matokeo yamefutwa.

"Kwenye Shule ya Twibhoki watahiniwa walikuwa 67 lakini 66 walifanana majibu kwenye mitihani lakini mmoja alijibu kivyake hajafutiwa, uchunguzi unaendelea katika Shule ya Twibhoki wapo watuhumiwa 12 wapo mahabusu kuna ushahidi wa kutosha kwamba walihusika na wizi wa mitihani,"alisema.

Alisema vituo hivyo viwili uchunguzi unaendelea ili kujua chanzo cha kuvunja mtihani kwa kuwa kunadaiwa kulikuwa na usimamizi usioridhisha. "Hatuwezi kuwa na watu wanaotuingiza kwenye gharama kama mtihani wa darasa la saba tulivyorudia tulitumia mabilioni ya fedha huu ni uhujumu uchumi kudanganya kwenye mitihani, polisi wanafanya uchunguzi tunaamini hatua zitachukuliwa na wizara imeridhika na hatua zilizochukuliwa na baraza," alisisitiza.

Kutokana na hali hiyo, alisema wazazi wanaohitaji maelezo zaidi kwa baraza na wizara, wako tayari kukutana nao na kuwaeleza. Pia alisema serikali itafanya mabadiliko ya sheria ili hatua zaidi zichukuliwe kwa wanaofanya udanganyifu kwenye mitihani na kuwa na ubora wa elimu.

HABARI KITAIFA



Ofisa wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu Kidakio cha Pwani, Halima Faraji, akipanda mti katika Bonde la Mto Mpiji, eneo la Mabwepande, Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa shughuli za upandaji miti kwa lengo la kuzilinda kingo za mito. Miti 1,500 imekwishapandwa katika kingo za mto huo. **PICHA: FRANK MONYO**

# NSSF yalipa bil. 2.6/- wenye vyeti feki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amesema katika nusu ya mwaka wa fedha uliyoishia Desemba, 2022, wamelipa Sh. bilioni 2.6 kwa watumishi 183 walifutiwa ajira kutokana na kosa la kughushi vyeti.

Mshomba alibainisha hayo jana jijini hapo, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mfuko na mwelekeo wa utendaji katika mwaka wa fedha 2022/23.

"Katika nusu ya mwaka wa fedha uliyoishia Desemba 2022, mfuko ulilipa mafao ya Sh. bilioni 350.7 kwa wanachama wastaafu na wanufaika wengine wapatao 80,339.

"Malipo haya yanajumuisha Sh. bilioni 2.6 zilizolipwa kwa watumishi 183 waliofutiwa ajira kwa kukosa vyeti halali baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuelekeza watumishi hao kulipwa mafao ya michango waliyochangia katika kipindi cha ajira zao," alisema.

Pia alisema katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 2023, mfuko unatarajia kulipa mafao yenye thamani ya Sh. bilioni 769.3 ambayo ni ongezeko la asilimia 17 kulinganisha na Sh. bilioni 659.8 zilizolipwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2022.

"Katika eneo hili la mafao napenda kumshukuru tena Rais kwa kuridhia ombi la vyama vya wafanyakazi kupitia TUCTA (Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi la kuja na kikokotoo kipya kwa ajili ya manufaa ya wastaafu wetu ambacho kilianza kutumika Julai, 2022," alisema Mshomba.

Pia alisema kutokana na hali hiyo, sasa wastaafu wanapokea mkupuo wa awali wa asilimia 33 kulinganisha na asilimia 25 ambayo wastaafu wa NSSF walikuwa wanapata.

"Jambo la msingi hapa ni kwamba kikokotoo hiki kinazingatia uendelevu wa mifuko yetu ya hifadhi ya jamii," alisema.

Kadhalika, alisema katika nusu ya mwaka iliyoishia Desemba, 2022 mfuko uliwekeza Sh. bilioni 483 katika uwekezaji mpya ukijumuisha hatifungani, amana za benki, dhamana kwa kampuni.

Uwekezaji huo, alisema ulihusisha pia miradi ya ujenzi na uwekezaji katika kiwanda cha sukari Mkulazi na kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 246 sawa na asilimia 51 ziliwekezwa katika hati fungani za serikali.

"Eneo hili ni salama, lenye faida kwa mfuko na taifa kwa ujumla kwa kuwa fedha hizi zinatumiwa na serikali kama fedha za ndani kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo," alisisitiza.

Kuhusu kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha sukali cha Mkulazi, alisema kinatarajiwa kuanza uzalishaji Julai, mwaka huu.

"Kiwanda hiki kinatarajiwa kupunguza changamoto ya uhaba wa sukari inayojitokeza mara kwa mara na kuilazimu serikali kutegemea wazalishaji na waagizaji binafsi kuzalisha na kuagiza sukari," alisema.

Alisema mradi huo unatarajiwa kutoa fursa ya soko kwa wakulima wa nje wanaolima miwa katika mashamba yenye takribani hekta 450, miundombinu mingine kwa ajili ya wananchi wanaozunguka mradi huo.

"Pia ajira zaidi ya 2,315 za moja kwa moja megawati 15 za umeme zinazotarajiwa kuingizwa katika gridi ya Taifa kupitia kituo cha kupokelea na kupoozea umeme Msamvu," alisema.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka na umefikia asilimia 75.

# Wabunge wacharuka ubadhirifu halmashauri

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE wametaka watumishi waliohusika na ubadhirifu katika halmashauri nne zilizotajwa kwenye ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kuwajibishwa haraka.

Wakichangia mjadala baada ya kamati kuwasilisha ripoti yake bungeni juzi, wabunge walisema kuendelea kuwaacha au kuwaamisha ni kulea wizi.

Mara kwa mara LAAC imekuwa ikiwasilisha taarifa za ubadhirifu ndani ya mamlaka za serikali za mitaa lakini hakuna mabadiliko wala hatua kuonyesha wahusika wanajirekebisha. Hatua hiyo imeelezwa kuwa kutokuchukuliwa hatua kumefanya matatizo hayo hasa wizi wa fedha kuendelea kuwa sugu.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamasi, alisema watumishi waliohusika katika wizi au ubadhirifu huo katika manispaa za Ubungo, Kigamboni, Ilemela na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, wanapewa barua za onyo, wanahamishwa na wanaanza kufanyiwa uchunguzi.

"Cha kushangaza zaidi, baadhi ya watumishi wapo halmashauri wakati bado wanafanyiwa uchunguzi. Wengine wanapelekwa polisi au TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Hawa ni wachache bado haitoi 'justification' (uthibitisho) kwa sababu ripoti ya CAG ina uzito wa kutumika kama ushahidi mahakamani," alisema.

Mbunge wa Igalula, Venant Daud, alisema wanavyosema ubadhirifu au mambo hayaendi sawa serikalini si wao wanasema bali wananchi.

"Katika ripoti zote CAG kila mwaka tunapokuja hapa hata hizi za kamati za fedha, hatuwezi kusema serikali imepoteza, kila siku tunapata hasara," alisema.

Alishauri serikali kupitia miradi mikubwa inayotafuta fedha ikiwamo ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na reli ya kisasa (SGR) kuwa kama hakutawekwa mipango madhubuti ya usimamizi wa fedha hata, hizo zitakuja kukaguliwa na kuambiwa zimepigwa.

Pia alisema katika ripoti ya CAG kuna changamoto kubwa ya riba ambazo zinalipwa kutokana na kuchelewesha makandarasi iliyosababishwa na uzembe wa watumishi wa wizara na taasisi.

"Unakuta mkandarasi unamchelewesha malipo mpaka siku 205 na unalipa riba ya zaidi ya Sh. bilioni 11 halafu watu tunakuja hapa kumsema. Kama hatuwezi tujadili masuala ya uganga wa kienyeji, tukae kimya.

Niwaombe wabunge tusipojisimamia sisi wenyewe kuna siku itakuja mtukanwe na bado mkapiga makofi," alisema.


# Notice

pwc

**PricewaterhouseCoopers (PwC) - clarification of Companies Act notice**

Newspaper notices in the 7 February 2023 editions of The Guardian and Nipashe included a winding up notice in relation to PricewaterhouseCoopers Services Limited. This company is a dormant company which is now being put into liquidation as it is no longer operational.

This notice does not relate to either of our two active entities, PricewaterhouseCoopers (partnership) and PricewaterhouseCoopers Limited, which operate as normal. Indeed, we continue to invest for the future, building on the legacy we have set in the country since 1947 (then Cooper Brothers and Company, later Coopers & Lybrand (in 1957), and now PricewaterhouseCoopers (since 1998)). For further information do visit www.pwc.co.tz, or contact us at info@pwc.co.tz

© 2023 PricewaterhouseCoopers Limited. All rights reserved. In this document, "PwC" refers to PricewaterhouseCoopers Limited which is a member firm of PricewaterhouseCoopers International Limited, each member firm of which is a separate legal entity.



Meneja Uhusiano Airtel Tanzania, Jackson Mmbando (kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kutangaza kutoa faida ya sh bilioni 1.6 kwa wateja na mawakala waliokuwa wakitumia huduma ya Airtel Money kwa kipindi cha Julai mpaka Septemba 2022. Faida hiyo, imekuwa ikitolewa kwa wateja na mawakala, baada ya kuidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Airtel Money, Daudi Ndovu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Binti aliyeuawa na kakaye azikwa kwa heshima

**Na Jenifer Gilla**

MAMIA ya waombolezaji, jana walishiriki maziko ya Anna Thomas (28) aliyeuawa na kaka yake wa kufikia, Erick Kwai (32) kwa kuchomwa visu shingoni na kisha kuutumbukiza mwili wake kwenye shimo choo.

Anna alikutwa na mauti Februari 4, mwaka huu, nyumbani kwao Mtaa wa Kimamba, Kata ya Makulumla, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam na alizikwa kwa taratibu za Kanisa Katoliki tofauti na kaka yake aliyezikwa juzi na Mchungaji Imani Katana aliyejitolea kuongoza ibada ya mazishi ambayo mama yake mzazi, Lonida Mosha awali aliyasusia.

Hata hivyo, baada ya majadiliano ya kina alikubali kumzika mwanawe kwa shingo upande huku akiwa haonyeshi majonzi yoyote.

Siku ya tukio, mama huyo alichomwa kisu na mwanawe Erick baada ya kufika nyumbani na kuuliza aliko Anna ndipo alielekezwa na wakati anaingia alishambuliwa na kisu huku majirani walipoona walikasirika, wakampiga kijana huyo hadi kufariki dunia.

Binti huyo wa kufikia ambaye ameishi na mama huyo kwa takriban miaka 17, tangu awali Lonida alisema hataki kurudi tena kwao kwa kuwa alivyorudi alikuta wazazi wake wote wamefariki dunia na hakuna wa kumjali, hivyo siku akifa azikwe Dar es Salaam.

**HALI ILIVYOKUWA**

Jana, mama wa Erick alikuwa mwenye majonzi mengi akimlilia Anna huku akisaidiwa na waombolezaji, tofauti na wakati wa mazishi ya mwanawe wa kumzaa. Pia hakuweka msiba nyumbani kwake na tangu awali aliwaeleza waandishi wa habari kuwa mwanawe huyo azikwe na manispaa.

Mama huyo alisema atamlilia Anna kwa kuwa ndiye mwanawe aliyeishi naye tangu alipomwokota Kituo cha Mabasi Ubungo, huku mwanawe wa kumzaa akimsumbua kutokana na kujihusisha na bangi.

Mwili wa Anna ulifikishwa katika Kanisa Katoliki, Parokia ya Parokia ya Familia Takatifu Mburahati saa 7:30 mchana ukiwa katika gari maalum ya kubebea maiti. Familia ilishiriki ibada ya mazishi wakati Erick alitafutiwa mchungaji kutoka Kanisa la Baptist huku akipelekwa makaburini kwa kutumia gari aina ya Canter.

Muda wote wa mazishi, mama mlezi wa binti huyo, Lonida aligubikwa na huzuni, alisikika akilia na kuomboleza hadi kufikia hatua ya kuishiwa nguvu, hivyo ndugu kulazimika kumsaidia jambo ambalo halikutokea katika mazishi ya kijana wake, Erick.

Aidha, watoto watatu wa Lorina ambao ni ndugu wa kuzaliwa wa Erick, jana walivaa sare nyeusi na kulibeba jeneza lenye mwili wa Anna muda wote ilipohitajika kufanyika hivyo tofauti na mazishi ya mdogo wao.

Wakati wa kuaga mwili wa Anna, vilio vilitawala kutoka kwa waombolezaji huku kila mmoja akiomboleza kwa namna alivyomfahamu huku wengi wakisema alikuwa binti mpole na mwenye upendo kwa watu wote.

Mwili wa Anna ulipelekwa makaburini saa 9:15 alasiri na kupokewa na umati wa watu, wengi wakiwa vijana waliokuwa wakiimba nyimbo za kuomboleza kipindi chote cha kuuzika pembeni ya alipozikwa Erick.

**NENO LA PAROKO**

Akitoa neno wakati akiongoza misa hiyo, Padri Vitalis Kasembo aliwasihi waombolezaji kumshukuru Mungu kwa kila jambo kwa kuwa yote yanayotokea ni mapenzi yake na njia ya kuwafanya wanadamu waendelee kuona ukuu wake.

Akisoma historia ya marehemu, kaka wa kufikia, Joseph Kwai, alisema alizaliwa mwaka 1997 mkoani Mwanza, akapata sakramenti ya ubatizo mkoani humo mwaka 1998 na kipaimara mwana 2010. Alimaliza elimu ya msingi mwaka 2012.

Alisema baada ya kumaliza elimu Anna alikwenda Dar es Salaam ndipo alipokutana na familia ya Kwai na kuishi nao kama mtoto wao mpaka umauti ulipomkuta Februari 4, mwaka huu.


## OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Huduma ya Chakula

## REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0113

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za Ujenzi wa Gati na kituo cha kupakia katika Ghuba ya Tanga kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inawaalika watoa huduma kueleza nia yao kwa utoaji wa:

**- Huduma ya Chakula**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Kuandaa na Kupeleka kwenye ofisi za BBN Limited Mlo kamili au chakula cha mchana cha wafanyakazi kila siku za Jumatatu hadi Jumamosi.
- Mtoa huduma atakuwa na jukumu la kuandaa menyu ya chakula ya wiki nzima na kuiwakilisha kwa BBN ili kuwa na mpango wa milo ya wiki nzima itakayokubaliwa kwa pamoja.
- Mkataba/kandarasi itakuwa ya kipindi cha MWAKA MMOJA kutoka ya tarehe ya kuanza kwa utoaji wa huduma ya chakula na uwezekano wa kuongeza muda.
- Mkandarasi kwa nyakati zote atatakiwa kuzingatia viwango vya ubora na vipengele ikiwa ni pamoja na usafi katika upishi na uandaaji wa chakula, kuzingatia ratiba na muda wa chakula pamoja na matumizi salama na njia bora za usafiri.
- Mtoa Huduma atawajibika na utunzaji na uingizwaji wa vyombo vitakavyotumika ikiwa kutakuwa na upotevu au uvunjifu.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Huu ni wito kwa kuonyesha maslahi au nia (EOI) umekusudiwa kutoa muongozo kwa watoa huduma kuonyesha uwezo na uzoefu kwa kutoa huduma ya chakula kwa namna itakayokidhi matarajio ya BBN Limited.
- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo kutekeleza kandarasi husika.
- Cheti au Hati safi ya mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Kutoa uthibitisho wa leseni kutoka kwenye Mamlaka za usimamizi na udhibiti wa chakula au utoaji huduma ya chakula.
- Wasifu wa kampuni ukionyesha ya uzoefu wa kutosha katika biashara ya upishi au huduma ya chakula
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **23 Februari 2023 , Saa 12;00** majira ya Tanzania.

Kichwa au Mada ya barua pepe inapaswa kuwa: **ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0113** (Nambari ya kumbukumbu ya EOI iliyotajwa kwenye kichwa cha Tangazo hili)

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu, yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.


# Mchakato kupitia sheria kandamizi waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila, ili kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane kwenye mirathi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali inawasaidiaje wajane ili kuondoa mila na desturi potofu zinazo mkandamiza mwanamke kwenye mirathi.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema serikali inatambua uwepo wa wajane na katika kulinda haki zao kwa kutunga sheria mbalimbali na kanuni za kulinda haki za wanawake katika suala zima la mirathi.

"Suala la mila na desturi potofu ni eneo ambalo serikali imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila, ili kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane katika suala la mirathi. Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu sheria ya mirathi hususan umuhimu wa kuandika wosia katika kuondoa changamoto zinazotokana na mila na desturi potofu," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuajiri wanasheria, ili kusaidia kutoa elimu ngazi ya kata kutoa elimu ya mirathi.

"Inasikitisha na kuona huzuni wanawake wajane wamejikunja hawajui hatima yao kwasababu wanadhurumiwa haki yao ya mirathi serikali ina mpango gani wa kuleta sheria ili kuondokana na tatizo hili," alisema.

Akijibu maswali hayo, Pinda alisema mtu anapopewa nafasi ya kuwa msimamizi wa mirathi anajiona ni mrithi wakati yeye sio mrithi anatakiwa kusimamia warithi kupata haki zao.

"Kwa sasa mtu akipewa nafasi anaanza kujinufaisha mwenyewe huyu ni mrithi anatakiwa kushtakiwa, kinamama wananyanyasika kutokana na mashemeji waliopewa jukumu la kusimamia mirathi kula mali za marehemu," alisema.

Aidha, alisema kuna mila zinafanya msimamizi wa mirathi kuwa na sauti kwa asilimia 100, lakini hilo halipo kisheria.

HABARI KITAIFA

# Lissu asimulia ubalozi wa Ujerumani walivyomwokoa

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema alikaa Ubalozi wa Ujerumani Tanzania kwa siku nane baada ya kunusurika kutiwa mikononi mwa watu waliotaka kumdhuru.

Lissu ambaye mwaka 2017 alipigwa risasi 32 kati yake 16 zilimpata mwilini, aliyasema hayo juzi Ikungi mkoani Singida wakati akihutubia mamia ya wananchi waliojitokeza.

Kiongozi huyo yuko kwenye ziara Singida na alielezea pia maisha aliyopitia tangu apigwe risasi, alivyotibiwa Kenya na Ubeligiji pamoja na alivyorudi kushiriki uchaguzi mkuu mwaka 2020 na kuondoka chini ya uangalizi wa Balozi wa Ujerumani.

Alisema baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, alipenyezewa taarifa na msamaria mwema (ambaye hakumtaja) za kufanyiwa fujo kwa mara ya pili.

Lissu ambaye ni mwanasheria kitaaluma na aliyewahi kuwa Mbunge wa Singida Mashariki, alisema mtoa taarifa alimjulisha kuwa waliokuwa wameamrishwa kumtendea tukio hilo, waliambiwa wasikosee kama walivyokosea kwenye tukio la mara ya kwanza Septemba 7, 2017.

"Nilipata hizo taarifa kabla ya uchaguzi lakini kwa sababu ulikuwa unaangaliwa na mataifa mengi duniani waliotumwa hawakuweza kunifanyia hizo vurugu wakati huo.

"Baada ya uchaguzi wakaanza mkakati wa kutekeleza hiyo amri. Nikaenda mafichoni Oktoba 30, 2020 uchaguzi ulivyokwisha baada ya siku mbili. Kuna mtu akaniletea taarifa nilikokuwa nimejificha kwamba wameshajua ulikojificha kimbia. Nilikuwa mimi pamoja na walinzi wangu wanne ikabidi tukimbie, nikajiuliza sasa tunakimbia tunaenda wapi kwa sababu ninafahamiana na watu wengi nikawa natafuta nitaenda wapi kupata usalama wa maisha yangu kutafuta kwenye simu nikaipata namba ya Balozi wa Ujerumani," alisema.

Lissu alisema baada ya kuambiwa maneno hayo alimtumia ujumbe balozi huyo na kumwambia "Kuna watu wananifutilia nakuja ubalozini kwako kwa ajili ya kupata hifadhi."

Alisema baada ya hapo walitoka mbio kwenda kwenye jengo hilo na walipofika kabla hawajaingia ndani, walinzi walimuuliza kama ana ahadi na balozi na akawajibu hana lakini anaomba ruhusa ya kuingia.

"Walinzi wakasema ngoja tuulize kwanza. Wakati wanauliza yakaja magari matatu yakafunga barabara upande mmoja na upande wa pili halafu wakashuka watu wakanifuata nilipo wakiwa hawana sare wala vitambulisho.

"Wakaniambia Mheshimiwa Lissu, tunakuhitaji Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, nikawauliza nyie ni kina nani? Wakasema wao ni polisi, nikawauliza nina kosa gani? Wakasema hawajui lakini wameambiwa waje wanikamate na kunipeleka huko.

"Wakati tunaendelea kubishana huku wanataka kuniingiza kwenye 'defender' (gari ya polisi) lao na huu mguu wangu haupo salama, bahati nzuri geti la Ubalozi wa Ujerumani likafunguliwa akatoka Naibu Balozi (hakumtaja jina) na maofisa wake wawili wakawauliza wale polisi mnampeleka wapi? Sisi tumemwalika aje kula chakula cha jioni nasi hapa ubalozini. Hakukuwa na chakula chochote nilikuwa nakimbia, sasa ikawa wale polisi wanawaambiaje wale wazungu," alibainisha.

Alisema baada ya wale polisi kung'ang'ania kuondoka naye, yule Naibu Balozi aliwauliza kama yeye na wenzake wanaweza kwenda kwenye hayo mahojiano? Polisi wakamjibu inawezekana badala ya kuingizwa kwenye gari la polisi, alitumia gari lake na wale maofisa ubalozi wakaongozana nao mpaka polisi.

Kwa mujibu wa Lissu, walipofika, Naibu Balozi aliwauliza watakuwa naye muda gani ndipo wakajibu dakika 20 akawaambia zikifika hizo dakika wamruhusu kwa kuwa wanataka kwenda naye kula chakula.

"Giza lilishaanza kuingia wakamwambia alipo hayuko salama wakitaka nirudi ubalozini wataniachia niende mwenyewe. Yule balozi aliwajibu kama siwezi kuwa salama nikiwa kwenye kituo cha polisi siwezi kuwa salama sehemu nyingine yoyote hapa hatuwezi kuondoka.

"Ikabidi huko ndani waniambie sasa wewe tulitaka kuzungumza kidogo sasa unaleta wazungu, ikabidi waniachie na yule balozi akaniambia hii nchi si salama kwako inabidi ukae ubalozini kwangu mpaka utakapopata namna ya kusafiri.

"Nilikaa siku nane ubalozini kwao wakasimamia nikapata hati ya kusafiria na yule mama alinisindikiza mpaka kwenye ndege akasema maadamu umeingia humo tunaamini hapo uko salama ndio sababu mpaka leo hii nipo hai," alisema Lissu.

Lissu alirejea nchini Januari 25, mwaka huu, akitokea Ubelgiji alikokuwa kwenye matibabu baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kufuta zuio la vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, huku Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, akiliambia Bunge kuwa nchi ni salama na walioko nje wanaweza kurejea.

# Zumaridi huru kesi usafirishaji binadamu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MCHUNGAJI Diana Bundala, maarufu kama Mfalme Zumaridi, ameachiwa huru katika kesi iliyokuwa ikimkabili ya usafirishaji haramu wa binadamu baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kudai kuwa hana nia ya kuendelea nayo.

Kutokana na madai hayo, ameomba shauri hilo kuondolewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza.

Shauri hilo lililokuwa limepangwa kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya mashahidi ili kwenda Mahakama Kuu kusikilizwa ushahidi wake Februari 9, mwaka huu, lilisikilizwa kwa dharura jana katika chemba ndogo ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Boniventure Lema.

Akisoma uamuzi huo, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Dorcus Akyoo, alisema DPP alifikia uamuzi huo kutokana na kifungu cha sheria namba 90 kifungu kidogo namba 11 Sura ya 20 ya Mwenendo wa Mashahidi kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Lema alimwachia huru Zumaridi katika kesi hiyo namba 11/2022.

"Sasa uko huru katika kesi hii namba 11/2022, hivyo unaweza kuendelea na shughuli zako lakini hii haitoathiri shauri lilokuweka hatiani," alisema Lema.

Baada ya uamuzi huo, Wakili aliiomba mahakama kupokea maombi ya serikali juu ya kuomba awe chini ya uangalizi katika kipindi cha miaka mitatu bila kujihusisha na masuala yoyote ya uvunjifu wa sheria na amani katika maeneo yake sambamba na kuripoti kwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa (RCO) wa Mwanza mara moja kila mwezi.

Alisema maombi hayo yalitolewa chini ya kifungu cha sheria namba 70 na 72 kifungu kidogo 'e' pamoja na kifungu namba 74 na 370 kifungu kidogo 'a' cha mwenendo wa makosa ya jinai sura namba 20 na kusema kuwa maombi hayo yameambatana na kiapo cha mkuu wa upelelezi wa mkoa wa Mwanza RCO.

"Tunaomba hayo kutokana na mjibu maombi kushtakiwa katika shauri namba 11/2022 la kusafirisha binadamu kinyume cha sheria chini ya kifungu namba 4 kifungu kidogo namba 1 (a) na kifungu namba 6 kifungu kidogo namba 11 (a) cha Sheria ya Udhibiti wa Usafirishaji Haramu ya mwaka 2016 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021/22.

Kutokana na sheria hiyo, alimtaka Zumaridi kuweka saini na kukubali maombi hayo mbele ya mahakama na kuahidi kuwa mwenye tabia nzuri, atatunza amani na hatosababisha fujo yoyote kwa kipindi hicho cha miaka mitatu.

Saa 8:23, Hakimu Lema aliahirisha kikao hicho kwa muda wa dakika 30 kumpa nafasi Zumaridi kujifikiria na kutoa uamuzi kama atakubaliana nayo bila kuwapo kwa wakili utetezi kutokana na shauri hilo kuitwa kwa dharura.

Baada ya kurejea katika kikao hicho, upande wa utetezi ulifika na wakili wa utetezi, Erick Muta, na kukubaliana na baadhi ya maombi kwa njia ya mdomo huku akieleza kuwa baadhi ya maombi yaliyotolewa yanaondoa haki ya msingi ya kikatiba ya kuwa huru kutokana na maombi hayo kujengwa katika msingi wa shaka na hofu na kumnyima mpokea maombi kuwa huru wakati wa maisha yake uraiani.

Wakili Akyoo alidai lengo la kufikisha ombi hilo ni kwa ajili ya kumfanya mjibu maombi (Zumaridi) asijihusishe na vitendo ambavyo awali alishtakiwa nayo.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Lema aliahirisha utolewaji wa majibu ya maombi hayo huku akiwataka kurejea mahakamani Februari 14 kwa ajili ya kusikiliza majibu ya maombi hayo.

Pamoja na kuachiwa huru, Zumaridi anaendelea kutumikia kifungo cha mwezi mmoja na zimesalia siku 10 kumaliza.


TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA

SHELLS TANZANIA LIMITED

Cheti cha Usajili No. 16839

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni la Shell Tanzania Limited Limited, yenye usajili namba 16839 kitakachofanyika tarehe 15 Machi 2023 ofisini kwa mfilisi saa 4:00 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | JOSEPH LYIMO |
| Amwani ya Mfilisi | PricewaterhouseCoopers Limited, Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay. P.O. Box 45. Dar es Salaam. Tanzania |

| | |
|---|---|
| Tarehe ya kuchaguliwa | 1 November 2021 |
| Amechaguliwa na | WAMILIKI WA KAMPUNI |

Sahihi ...................... Tarehe: 30/01/2023

Jina: JOSEPH LYIMO

Imetolewa na:

JOSEPH LYIMO

SHELL TANZANIA LIMITED

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua madhubuti zichukuliwe kwa wanaohusika na ubadhirifu

**KAMATI** ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), juzi iliwasilisha taarifa Bungeni inayoonyesha kuwapo kwa ufisadi wa kutisha wa mabilioni ya shilingi katika baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa nchini. Katika taarifa hizo, manispaa za Ubungo, Kigamboni na Ilemela pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, zilitajwa kuwa vinara katika ubadhirifu huo.

Taarifa ya kamati hiyo ilibainisha kuwa katika baadhi ya halmashauri, kuliibuliwa madudu kwenye ukusanyaji mapato huku taarifa zikichakachuliwa na kuwekwa tarakimu ambazo si sahihi. Pia malipo katika baadhi ya miamala haikuwa sahihi huku maofisa masuhuli wakishindwa kudhibiti hali hiyo.

Kutokana na kuwapo kwa madudu hayo, baadhi ya wabunge, wakichangia mjadala wa taarifa hiyo, walikuja juu huku wakitaka wale wote waliohusika na ubadhirifu huo, wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria, kwa maana ya kusimamishwa, kuchunguzwa na wale watakaobainika wapelekwe kwenye vyombo vya sheria na kushtakiwa.

Baadhi ya wabunge katika kuchangia kwao, walisema taarifa za namna hiyo za kamati pamoja na zile za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kila mwaka zimekuwa zikiibua madudu hayo na kwa kiasi kikubwa hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa dhidi yao.

Kujirudia kila mwaka kwa mambo hayo, inaonekana dhahiri kwamba ni mchezo uliozoeleka miongoni mwa watumishi na wanaona ni kawaida yao kufanya hivyo kwa kuwa hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi ya wanaohusika.

Mamlaka za serikali za mitaa, kwa maana ya halmashauri za majiji, manispaa, miji na wilaya, ndizo watekelezaji wakuu wa miradi ya serikali kama vile afya, barabara, maji, elimu na ile ya kiuchumi kama vile kilimo na ufugaji. Kutokana na ukweli huo, fedha nyingi kutoka serikali kuu na zile zinazotokana na makusanyo ya ndani, huelekezwa huko kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Pamoja na nia nzuri ya serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo, baadhi ya mafungu ya fedha za maendeleo yamekuwa yakiingia mifukoni mwa wajanja - watumishi wa halmashauri walio waaminifu na matokeo yake wananchi kuitupia lawama serikali. Swali la kujiuliza ni kwamba sekretarieti za mikoa zinafanya nini kudhibiti wimbi hilo la upigaji wa mabilioni ya miradi ya serikali?

Taarifa ya LAAC iwe kengele ya kuiamsha serikali na kuchukua hatua dhidi ya wahusika wote waliotajwa katika kashfa za ubadhirifu na upigaji wa mabilioni hayo ambayo yalilenga kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbalimbali.

Jambo la msingi ni kwamba serikali kuu, kupitia mamlaka za uteuzi wa wakurugenzi na ajira kwa wakuu wa idara na vitendo, zichukue hatua dhidi ya wale wanaohusika na kashfa hizo ambazo zinaitia doa serikali kuwa ndani mwake kumejaa wezi na wabadhirifu. Pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inapaswa kuingia kazini kuwachunguza wote wanaotuhumiwa kuhusika na kashfa hizo.

Ni vyema wale walioteuliwa katika nafasi ya ukurugenzi, kama wanatajwa kuhusika ni vyema wakatenguliwa ili iwe fundisho kwa wengine. Ni imani kwamba iwapo hatua hiyo itachukuliwa pamoja na baadhi ya wakuu wa mikoa na maofisa masuhuli, kwa maana ya makatibu tawala wa mikoa kutikiswa, mchezo huo utapata dawa maridhawa na hatimaye uhalisia wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika serikali utaonekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kijiji hiki kisaidiwe kukabiliana na uvamzi huu wa tembo usikoma

Na Halfani Chusi

**NILISIKIA** wakazi wa Kata ya Namapwiya na nyingine tatu wilayani Nachingwea hivi karibuni, kutoka mkoani Lindi wanalia njaa kutokana na uharibifu wa tembo, hata kuhemea mazao ya mizizi.

Hadi serikali kitaifa, ikipatoa mamlaka za kimkoa, inachukua hatua kuwapo kiasi kikubwa cha chakula cha nafaka kimeagizwa kutoka mkoani Ruvuma, kuwakimu wakazi hao. Sio taarifa nzuri kitaifa.

Wakazi hao walianza kupata shida hiyo tangu Agosti mwaka jana, baada ya tembo kuvamia mashamba yao na kuharibu mazao, wakiibukia jirani kwao hifadhini Selous, ambako hali si nzuri.

Kimsingi, uvamizi huo wa tembo umekuwa wa kila mara na hakuna suluhisho la kudumu tunalolisikia na msukosuko huo si wa wana - Nachingwea peke yao.

Mkoani Iringa nalo ni yaleyale kijijini Mgowelo, katika wilaya ya Kilolo Kata ya Nyanzwa, wakazi wake nao wako kwenye kiza kinene kutokana na adha wanayoipata dhidi ya tembo wanaovamia mashamba yao na kuteketeza mazao.

Si mara moja tembo kuvamia kijiji hicho na kuteketeza mazao ya wakulima ni jambo ambalo wanakijiji hao wamekuwa wakilipigia kelele kwa muda mrefu, huku utatuzi wake ukikabiliwa na kigugumizi.

Wanakijiji hao wamekuwa wakitoa malalamiko kwenye ngazi mbalimbali serikalini, lakini mara nyingi juhudi hizo zimekuwa hasara hazizai matunda, kutokana na suala hilo linaloutia umma hasa kuwa endelevu.

Kila mwaka, matukio dhidi ya tembo kuvamia mashamba na kuharibu mazao katika kijiji hicho yamekuwa yakitikisa. Ni adha isiyotoa hata mapumziko kwa wakulima.

Kuna haja sasa serikali kuingilia kati na kuweka mikakati endelevu dhidi ya tembo kwenye kijiji hicho na sio kuweka kambi kwa muda mfupi na kuondoka kama walivyokuwa wakifanya huko nyuma.

Hilo halisaidii kwa maana kwamba wanapishana tu na tembo, wanakijiji wanasema 'wanapokuwa wameweka kambi, tembo huwa hawaji, lakini wakishatoka tu tembo wanakuja!'

Siku chache zilizopita tembo walivamia kwenye mashamba ya wakulima kadhaa kwenye kijiji hicho na kuteketeza hekta kadhaa za mashamba ya ndizi na miwa, hali iliyowaachia simanzi na vilio wakulima huko kijijini.

Ikumbukwe uhalisia uliopo, tembo wanapovamia eneo fulani mbali na uharibifu wa mazao pia huchangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchafuzi wa mazingira wakati mwingine hata kuweka maisha ya wakazi rehani.

Mwaka jana wakazi wa kijijini hapo wilayani Kilolo, walikuwa wanalazimika kwenda kulala shambani kukabili tembo wasidhuru mazao yao, bila ya kujua kwamba wanaweka maisha yao rehani.

Tembo anapotambua kuna 'adui' watu wanalinda, anakuwa mnyama hatari na mbaya zaidi, akihisi kuwa sio rahisi mkulima kumdhibiti asiharibu mazao hayo.

Suala sasa linapaswa kutazamwa kwa ukubwa wake, ili kunusuru tembo wasidhuriwe na wananchi na wananchi kudhurika na tembo. Nakumbuka mwaka 2018, kuliripotiwa tukio la mtu aliyenusurika kufa kwa tembo, baada ya kuingia na kujificha chini ya daraja.

Kwa mtazamo huo hata wakazi kijiji hapo wapo hatarini kupoteza maisha dhidi ya tembo, ambao huingia mashambani mwa wakulima wakifuata ndizi na miwa kuanzia saa moja jioni mpaka saa 11.00 kumi na moja alfajiri.

"Tembo wakivamia shamba lazima wakuache mtupu, sasa ukiangalia kipato chenyewe huwa tunapata kidogo tena tembo wakiingia ndio kabisa huwa tunakufa njaa," anaeleza makazi Zika Paulo.

Mkazi mwingine, Enock Mbogo, anaishauri serikali pamoja na mamlaka husika, ziangalie namna ya kuwalipa fidia walioharibiwa mazao yao.

"Watu wanaharibiwa mazao yao na tembo, lakini fidia hawapewi na wengine waliahidiwa tokea muda mrefu lakini mpaka leo hawajalipwa kwa hiyo, tunaomba serikali iwaangalie waathirika hao hali ni ngumu," anashauri.

**Simu:+255 787879707**

HABARI KITAIFA

# PIC yapongeza maboresho ya bandari

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imesema mabadiliko ya menejimenti ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) yameongeza ufanisi wa mamlaka, huku ikishauri kuharakishwa mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jerry Silaa aliyasema hayo bungeni juzi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na kamati hiyo kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari 2023.

Alisema bandari hiyo inatarajiwa kuwa na vigezo vya kimataifa, hivyo kuongeza ushindani wa Bandari katika soko na kupata tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Aidha, alipongeza Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa inaendelea kupanuliwa kwa kuongeza gati na kina kwa ajili ya meli kutia nanga kwa ajili ya kushusha shehena za mizigo.

"Kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 bandari hii imepokea na kupitisha mizigo tani milioni 10.4 ambayo ni rekodi ya juu tangu kuanzishwa kwake, hivyo kusababisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) nayo kuvunja rekodi ya mapato kwa kukusanya Sh. trilioni 11.6. Katika makusanyo ya TRA, asilimia 41 ya ushuru wa forodha yanatokana na huduma zinazotolewa na TPA,"alisema.

Alisema bandari hiyo ndiyo lango la uchumi kwa nchi nyingi za kusini na mashariki mwa Afrika zikiwapo Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Uganda, Zambia, Uganda, Zimbambwe na Sudan Kusini ambazo zinatumia bandari hiyo kupitisha mizigo yao.

"Kwa kuwa upanuzi wa bandari hiyo unaoendelea sasa hautaweza kumaliza changamoto iliyokuwapo sasa ya wingi wa shehena zinazohudumiwa na nyingine kushindwa kushushwa kutokana na eneo kuwa dogo na kina kidogo.

"Bunge linaazimia kwamba serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ihakikishe inamaliza kwa haraka changamoto zinazozuia kuanza kufanya kazi kwa bandari kavu ya Kwala kwa kuwa hadi sasa bandari hii imekamilika kwa asilimia 98.

"Kwa kuanza kufanya kwa bandari hii itaongeza ufanisi na kiasi cha shehena itakayohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza msongamano wa shehena ya mzigo kwa asilimia 30,"alisema.

Katika hatua nyingine, Silaa alishauri kuanzishwe Mfuko Maalum wa Uwekezaji (Investment Fund) ambao utasaidia taasisi na mashirika ya umma yenye uhitaji wa haraka na ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kutoa huduma pindi inapohitajika.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange (wa tano kushoto), akisikiliza maelezo ya uboreshaji wa huduma za maji katika Mji wa Kigamboni kwa Mkurugenzi wa Uwekezaji na Miradi DAWASA, Mhandisi Ramadhan Mtindasi (kulia), wakati bodi hiyo ilipofanya ziara ya kukagua mradi wa maji Kigamboni juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Aweso akemea udanganyifu uunganishaji huduma ya maji

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameelezea kukerwa na udanganyifu katika kuunganisha mabomba ya maji na kuwataka watumishi kuacha mtindo huo.

Aweso alisema hayo jana wakati wa mkutano mkuu wa sekta ya maji uliofanyika jijini hapo kwa kushirikisha wafanyakazi wa sekta hiyo kutoka maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Aweso, kumekuwa na udanganyifu mkubwa mafundi

wanapowahudumia wateja hususani katika uunganishaji maji, huku akitaka tabia hiyo kuachwa haraka.

Alisema amekuwa akipata malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, hivyo anaomba suala hilo liachwe kabisa na wafanyakazi waendelee

kuwaunganishia maji wateja kwa bei halali na elekezi na sio vinginevyo.

Wananchi, alisema wanapaswa kupata maji safi na salama kwa sababu serikali imewekeza fedha nyingi katika sekta ya maji na kwamba ni muhimu wafanyakazi wakawajibika kuhakikisha huduma hiyo inapatikana.

Aidha, Waziri Aweso aliwataka wahandisi na maofisa wa maji kuwajibika katika utendaji wao wa kazi na kuhakikisha idara hiyo inafanya vizuri wakati wote kwa kushirikiana na wananchi kiutendaji

ili kurahisisha kufanikishwa kwa miradi.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Balozi Morocco ataja sababu zitakazoongeza watalii nchini

**Na Christina Mwakangale**

UKARIMU, chakula, mahala pazuri pa kupumzikia, upekee wa vivutio vya utalii na kuvitangaza, zimetajwa kuwa sababu za kuongeza watalii kwenye nchi yoyote.

Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri, alidokeza hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo uzoefu wa sekta ya utalii nchini mwake.

Alisema kwa mwaka, Morocco hupokea watalii kati ya milioni 12 huku ikishuka mwaka 2019 na kufikia milioni 10 kutokana na sababu ya UVIKO-19 ugonjwa ambao uliitikisa sekta hiyo duniani kote

Kwa mujibu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Tanzania ilipokea watalii 788,933 mwaka 2021 kutoka 562,549 mwaka 2020. Akifafanua zaidi kuhusu uzoefu wa nchi yake, alisema: "Kwenye utalii mikakati ya utalii iliyoko Morocco tuna bidhaa ambazo zinatuuza mfano fukwe miji, ambako kuna eneo lina upekee wake tofauti na maeneo mengine duniani.

Balozi Zakaria alisema diaspora walioko nje ya nchi, wanaweza kuwa mabalozi wazuri wa kutangaza utalii wa nchi wanazotoka huku akisema Wamorocco milioni tano wanaishi nje ya nchi na wamefanya kazi kubwa ya kutangaza utalii wa nchi yao.

"Idadi ya watu wa Morocco ni milioni 36 na Wamorocco milioni tano wako nje ya nchi. Hao pia ni mabalozi wazuri wakuitangaza nchi yetu. "Kinachotakiwa kuonyesha ni kile ulicho nacho kwa nchi nyingine na wageni. Mfano ni kujitangaza kwenye nchi zingine, tuna ofisi za utalii maeneo tofauti dunia kama Ulaya na Amerika Kusini.

"Kwenye utalii kwanza mtu anavutiwa na ukarimu, chakula kizuri mahala pazuri pa kupumzika, kulala," alisema mwanadiplomasia huyo.

Kadhalika, Balozi Zakaria alisema Morocco imekuwa ikibadilishana uzoefu na nchi za Afrika kuhusu mfumo wa kiteknolojia ili kasi ya maendeleo barani humo iende kwa pamoja.

"Wote ni waafrika bila kujali tofauti zetu za rangi, na pia kipaumbele chetu ni ushindani wenye fursa sawa, tuna usemi kwamba 'Africa by Africa for Africa' ndio kauli mbiu yetu," alisema Balozi Zakaria

Alisema wakati hivi sasa duniani bei ya bidhaa tofauti imekuwa ikiongezeka, ikiwamo mbolea, akisema Morocco imeshafanya mazungumzo na Tanzania, kuhusu ujenzi wa kiwanda cha bidhaa hiyo.

"Afrika ili kuhakikisha kuna amani, usalama wa chakula ni jambo muhimu. Tuna wawekezaji wengi ambao wanaweza wakaiona fursa Tanzania, ambayo imefunguliwa na serikali.

"Afrika inaweza kulisha dunia lakini haiwezi kujilisha yenyewe tunaposema usalama wa chakula maana yake ni mbolea imepanda, sisi Morocco tumeweka punguzo la mbolea.

"Tuna bara kubwa, wakulima na watu wanahitaji chakula. Afrika usalama wake ni kwenye chakula. Hatupendi kuona Watanzania, Waafrika kwa ujumla hawana chakula mezani, kulikuwa na mazungumzo na Serikali ya Tanzania tangu mwaka 2016, ili ikiwezekna kuwa na kiwanda kwa uhakika wa mbolea," alisema.



Mkuu mpya wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo (kushoto) akikabidhi rasmi ofisi kwa Mkuu mpya wa Wilaya ya Iringa, Veronica Kessy, mjini Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aagwa, amuuma sikio mrithi wake

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, ameagwa rasmi wilayani Iringa huku akimhimiza mrithi wake, Veronica Kessy, kuwabana maofisa wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wanaosimamia mradi wa machinjio ya kisasa.

Katika hafla ya kuagwa iliyofanyika Jumatatu wiki hii, Moyo alisema mradi huo mkubwa ni sehemu ya miradi itakayoongeza mapato ya halmashauri, pia utapanua soko la ajira kwa wafanyabiashara, wakiwamo wanajihusisha na biashara ya kitoweo.

Hafla hiyo ambayo pia iliambatana na kukabidhi ofisi, alimwomba Kessy ashughulikie changamoto ya kutokukamilika kwa wakati machinjio ya kisasa ya Ngelewala.

Alisema machinjio hayo ujenzi wake ulianza mwaka 2008 lakini hadi sasa bado hayajakamilika na yametumia zaidi ya Sh. bilioni mbili. Machinjio hayo yanatarajiwa kuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 200 kwa siku.

Moyo alisema kutokukamilika kwa machinjio hayo, kunatia dosari utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwa ujenzi umetumia zaidi ya miaka minane na bado hayajakamilika.

Moyo aliwaomba wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya, watumishi wa halmashauri zote za wilaya ya Iringa na wananchi, kumpa ushirikiano mkuu mpya wa wilaya. Alisema mafaniko aliyoyapata kwa kipindi alichokaa Iringa, ni matunda ya ushirikiano waliompatia, hivyo ni muhimu wakaendeleza ushirikiano huo kwa mkuu huyo mpya wa wilaya.

Kessy kwa upande wake aliahidi kuendeleza miradi iliyoachwa na mtangulizi wake na kusisitiza ushirikiano kwa kuwa ofisi yake iko wazi kupokea ushauri wenye lengo la kujenga na kuiletea maendeleo wilaya.

Alitumia nafasi hiyo pia kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan Kwa kuendelea kuwaamini yeye na mtangulizi wake kwa kuwapa nafasi ya kuwa wakuu wa wilaya huku akisema imani waliyopewa na Rais ni deni kwao, hivyo ni wajibu wao kumsaidia kikamilifu katika kufanikisha malengo ya serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kabla ya kuhamishiwa wilaya ya Iringa, Kessy alikuwa mkuu wa wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

# Muswada wa habari wasogezwa mbele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeahirisha kuwasilisha muswada wa marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari wa mwaka 2016 kwenye mkutano wa 10 wa bunge.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari, Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Gerson Msigwa, alisema serikali ilipanga kwenye mkutano huo kuwasilisha muswada wa mabadiliko ya sheria mbalimbali endapo ingetokea nafasi ikiwamo mabadiliko ya sheria hiyo.

"Jambo letu tulipanga kuwasilisha lakini ratiba ya bunge imebana sana hatukupata nafasi kwa hiyo tumeshindwa kuwasilisha muswada huu hadi kikao kijacho cha Mwezi Aprili ndio tunatarajia tutawasilisha muswada wetu,"alisema.

Alisema ratiba ya bunge imesababisha kushindwa kuwasilisha muswada huo na kwamba sio muswada huo, pia kuna miswada mingine haijawasilishwa kutokana na hali hiyo.

"Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote tumepata nafasi utawasilishwa na tuwaombee wabunge wetu watoe mawazo na ushauri nao upitishwe kwa kuwa kiu ya Rais ni muswada huu ukamilike haraka,"alisema Msigwa.



## DC aagiza vikundi kurejesha fedha za mikopo

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, ameviagiza vikundi vya wanawake na vijana waliopatiwa mikopo na Halmashauri ya Arusha, kurejesha fedha hizo kwa wakati ili ziweze kuwanufaisha watu wengine.

Alitoa agizo hilo jana, wakati wa hafla ya kukabidhi mkopo wa Sh.milioni 274 kwa vikundi 37 vya wanawake na vijana katika halmashauri hiyo.

"Wanavikundi ni vizuri mkatambua kuwa fedha hizi zinatakiwa kurejeshwa baada ya kipindi cha neema kupita. Ni vyema kuzitumia kwa kufanya miradi mliyoiandika kwenye maandiko yenu na kuzirejesha kwa wakati.

"Tukirejesha fedha hizi, kwa wakati kutatoa fursa ya kuwakopesha wengine na sisi wenyewe kukopeshwa kwa awamu nyingine, tumieni fedha hizi kwa nidhamu," alisema.

Aidha, aliwataka wanawake kuwahamasisha na kuwaelimsiha vijana ili waweze kunufaika na mikopo isiyo na riba inayotolewa na serikali kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri.

"Kinamama tuna jukumu la kuwaelimisha vijana wetu ili wajitokeze kwa wingi kuchukua mikopo hii, kwa kuwa vikundi vya vijana ni viwili tu, nina amini mikono ya wanawake inalea hivyo waleeni vijana, wajengeeni uwezo wa kufanya kazi kama nyie ili wanufaike na fursa hii adhimu," aliongeza.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema kwa kipindi cha miaka mitatu halmashauri hiyo imefanikiwa kutoa mikopo ya Sh. bilioni 1.3 na kwa kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha 2022/23 imekopesha Sh.milioni 509.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, ameipongeza halmashauri kwa kutekeleza Ilani ya CCM ya kupambana na umaskini kwa kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapa mikopo hiyo.

"Mikopo hii ni utekelezaji wa Ilani ya CCM, hivyo mnapaswa kuhakikisha mnaitumia vizuri iweze kuinua vipato vya familia pia tunategemea mkapambane na kuirejesha kwa wakati kulingana na utaratibu,"alisema mwenyekiti huyo wa CCM.

Awali Mkuu wa Wilaya alikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 274 kwa vikundi vya wanawake na vijana ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Habibu Malia, kijana mwenye ulemavu, aliishukuru serikali kwa mpango huo ambao utawasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi na aliwataka vijana kujitokeza kutumia fursa kuchukua mikopo hiyo.

# Moto wateketeza nyumba, kaya saba zalala nje

**Na Mary Mosha,** ROMBO

KAYA saba katika Kijiji cha Mbomai, Kata ya Tarakea-Motambu, Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, hazina mahali pa kuishi baada ya nyumba waliokuwa wakiishi yenye vyumba 11 kuteketea kwa moto.

Diwani wa Tarakea-Motambu, Felichism Oisso, alisema jana kuwa moto huo ulizuka usiku wa Februari 6 mwaka huu na kuathiri watu 32 waliopo kwenye kata hizo.

"Hakuna mtu aliyepoteza maisha, ila wananchi wamepoteza mali zao zote. Kwa sasa waathirika wa ajali hiyo wamehifadhiwa na wasamaria wema. Wamepoteza chakula, mavazi wanafunzi wamepoteza madaftari na wengine walikuwa na akiba ndani zimeteketea.

"Hatukufanikiwa kuokoa chochote na hii ni kutokana na kukosekana kwa gari la zimamoto pamoja na ubora wa miundombinu katika upangaji wa mji.

"Mji huu haupo kimpango na nyumba nyingi ni za mabanzi kutokana na ukosefu wa hati miliki. Tunaomba halmashauri ihakikishe mpango wa urasimishaji wa makazi unafanyika kwa wakati ili kuwaruhusu wananchi kupata hati miliki na kujenga nyumba za kudumu,"alisema Oisso.

Aidha, aliwataka viongozi wa serikali ngazi ya wilaya, kuhakikisha wanaleta msaada wa hali na mali katika kuokoa maisha ya wananchi hao waliopata majanga.

Mmoja wa waathirika wa ajali hiyo, Restuta Mzava, alisema moto huo ulianza katika maeneo ya paa kwenye chumba cha mpangaji mmoja, ambapo baada ya kubaini, walipiga kelele kuomba msaada bila mafanikio.

"Nyumba tuliokuwa tunaishi ni ya mbao, hushika moto kwa haraka, hatukuweza kuokoa chochote kutokana na watu wengi kuwa sokoni na aina ya nyumba hizi huteketea kwa haraka. Wanafunzi 20 wameunguliwa na kila kitu, wapo waliokuwa wameweka pesa ndani ikiwamo madalali wa viazi, vyakula na mavazi hivyo tunaiomba serikali kutusaidia misaada ya kibiadamu,"alisema Restituta.

Zaidi aliongeza, "Mimi nilikuwa na zaidi ya Sh.milioni 1.5 za kununua viazi, kwa wakulima ambazo zilikuwa chini ya godoro, zimeteketea zote. Tunaomba msaada ili tuweze kuendelea na maisha,"alisema Halifa Amiri.



Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Adam Kobelo (katikati), akifunga kikao cha baraza la mamlaka hiyo kilichojadili changamoto na mafanikio ya mji huo juzi. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo, Christopher Chengula na Ofisa Mtendaji wa Mji huo, Evence Mbogo. **PICHA: GIFT THADEY**

# EAC yazindua kituo cha kuwafunda vijana kuhusu amani

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC), imezindua kituo maalumu cha kuwafunda vijana kutoka jumuiya hiyo umuhimu wa kutunza amani katika mataifa yao.

Kituo hicho kilichojengwa jijini Arusha, kimepewa heshima ya jina la Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa kituo hicho, Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, alisema ujio wa kituo hicho ni sehemu ya mipango ya muda mrefu ya kuimarisha amani katika nchi za ukanda huo.

Alisema kituo hicho kimepewa jina la Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kama hatua ya kutambua mchango wake wa kutafuta na kudumisha amani enzi za uhai wake katika mataifa mbalimbali ya Afrika.


"Kwa sasa jitihada zimeanza kwa kuwashirikisha wadau katika uendeshaji wa kituo hiki. Tunaamini kitasaidia vijana kuthamini na kudumisha amani. Hawa watakuwa chachu ya kupunguza au kumaliza migogoro au vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi za jumuiya hii,"alisema.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na watendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Wawakilishi wa Baraza la Vyuo Vikuu Afrika Mashariki, wawakilishi wa vijana wa nchi zote wanachama na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali ili kuhakikisha kituo hicho kinatekeleza majukumu yake na malengo yaliyowekwa yanatimia.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Mtoto wa Hayati Mwalimu Nyerere, Makongoro Nyerere, alisema anajisikia fahari na mwenye bahati ya pekee kusikia na kuona mtazamo, malengo na matarajio ya Hayati Julius Nyerere yanafanyiwa kazi kwa vitendo, kitaifa na kimataifa.

Kwa mujibu wa rekodi za EAC, mipango ya kuanzishwa kwa kituo hicho ilianza tangu mwaka 2006.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# H'shauri yajenga chuo cha afya kuongeza wataalamu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imejenga chuo cha afya kwa ajili ya kuzalisha watumishi wa afya ambao watakwenda kutoa huduma katika zahanati na vituo vya afya ambavyo havina watumishi wa kutosha.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Charles Fussi, aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Fussi alikuwa akijibu hoja ya ukusanyaji wa mapato ya ndani iliyoibuliwa na Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma, alisema awamu ya pili ya mwaka 2022/2023 wametenga Sh.milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa chuo hicho.

Alisema halmashauri hiyo ilitenga Sh. milioni 400 katika mwaka wa fedha 2020/2021 na kujenga madarasa yenye uwezo wa kubeba wanafunzi zaidi ya 80, jengo la utawala pamoja na ofisi ya mkuu wa chuo.

Alisema wamekamilisha kwa wakati ujenzi wa zahanati 32 na vituo vya afya vitano, kati ya hivyo zahanati 16 hazina watumishi wa afya na Kituo cha Afya Mwalugulu.

"Lengo la ujenzi wa chuo hiki ilikuwa kiwe chanzo cha mapato cha halmashauri, lakini kiuhalisia haitakuwa rahisi kutokana na uendeshaji wake kuhitaji mapato makubwa, bali kitasaidia uzalishaji wa wauguzi watakaosaidia utendaji kazi katika vituo vya afya na zahanati kipindi cha kujifunza kwa vitendo," alisema Fussi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alisema, wamejenga chuo hicho kwa lengo la kupambana na uhaba wa watumishi wa idara ya afya.

Alisema chuo hicho kitaendeshwa na Wizara ya Afya kwa sababu wao hawana uwezo wa kukiendesha hususani katika kuwalipa watumishi ambao watakiendesha kituo hicho.

Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo Wizara ya Afya, Dk. Soitre Laizer, alisema amegiziwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kukagua ujenzi wa chuo hicho kama kimekidhi mahitaji ili kianze kutoa huduma.

Laizer alisema wako tayari kukiendesha chuo hicho endapo watakabidhiwa na halmashauri baada ya kukamilika na kuwataka kukamilisha majengo ya chumba cha TEHAMA, maktaba, mabweni na chumba maalumu kwa ajili ya kuhifadhi mitihani na mambo mengine.

Alisema kukamilika kwa chuo hicho kutasaidia kuondoa uhaba wa wauguzi katika vituo vya afya na zahanati hasa zilizopo pembezoni.

# Shule za bweni zatakiwa kuwakagua wanafunzi wakati wote

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

SHULE za sekondari za bweni zimetakiwa kuwa na utaratibu wa kufanya uchunguzi na ukaguzi wa mara kwa mara kwa wanafunzi wao ili kubaini na kudhibiti vitendo vya unyanyasaji wa kingono na ulawiti unaodaiwa kufanyika kwa kificho maeneo hayo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Dawati la Jinsia Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Mkaguzi wa Polisi, Grace Nyoni, wakati akitoa elimu ya namna ya kuepuka masuala ya unyanyasaji.

Elimu hiyo iliyotolewa kwa wanafunzi wa Sekondari ya Idetemya iliandaliwa Chuo cha Afya cha City ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum kwamba kila taasisi kuwa na mpango mkakati wa kupambana dhidi ya vitendo hivyo.

Nyoni alisema hatua hiyo itasaidia kubaini watoto wanaofanyiana vitendo hivyo wenyewe kwa wenyewe wale wanaofanyiwa majumbani kwao ili kuweza kuvidhibiti na kuwachukulia hatua wahusika.

"Dawati la jinsia katika vituo vyetu vya polisi liko wazi wakati wote leteni taarifa tutazifanyia kazi kwa wakati kudhibiti vitendo hivyo," alisema.

Akizungumza wakati wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi hao, Mkurugenzi wa chuo hicho, Zabibu Urasa, aliwataka wanafunzi kutoa taarifa wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia ili kusaidia wahusika wachukuliwe hatua.

"Vitendo hivi vinaanza kwa mtoto kushikwa sehemu mbalimbali za siri bila kujalisha jinsia yake, akikushika mtu yeyote sehemu hizo kataa na fikisha taarifa sehemu husika bila kujali hadhi yake," alisisitiza.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Idetemya, Matha Bathromeo, alisema shuleni hapo hawajapokea kesi yoyote ya ukatili wa kingono, lakini wapo karibu zaidi na maofisa ustawi wa jamii pamoja na dawati la jinsia wilayani humo ili kuhakikisha wanaripoti viashiria vitakavyojitokeza.

Elimu hiyo kwa wanafunzi iliambatana na matembezi ya hisani ya kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia sambamba na kutembelea na kutoa misaada ya chakula katika kituo cha marekebisho ya akili kilichoko wilayani Misungwi.

Kazi nyingine iliyofanyika ni kutoa misaada ya taulo za kike kwa wanafunzi wa shule hiyo pamoja na mahitaji mengine ya shule ikiwa ni sehemu ya kudumisha mahusiano na jamii.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi (katikati) na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ali Mwanga, wakikabidhi cherehani kwa kiongozi wa kikundi cha vijana, Rebeka John, wakati wa hafla ya kukabidhi hundi ya Sh. milioni 141 ya mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum, wilayani humo, mkoani Singida juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufungua tawi Kagera

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

WATAALAMU wa mradi wa The Higher Education for Economic Transformation (HEET) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wametua mkoani Kagera na kukutana na viongozi wa mkoa huo wakiwa na lengo la kuwashirikisha juu ya ujenzi wa chuo hicho mkoani humo.

Dk. Dotto Kuhenga ambaye ni miongoni mwa wataalamu wa HEET waliofika mkoani humo akiwasilisha wazo hilo kwenye Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, alisema dhumuni lao ni pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali juu ya utekelezaji wa mradi huo ili kuweza kutimiza malengo yaliyotarajiwa.

"Uendelezaji huu unadhaminiwa na Serikali chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mradi wa HEET chini ya Benki ya Dunia na ikumbukwe kuwa ujio wa mradi huu mkoani hapo utakuwa na faida katika mkoa pamoja na taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa chuoni," alisema Dk. Dotto.

Alisema kuwa miundombinu ya chuo hicho itakayojengwa ni pamoja na majengo ya madarasa, ofisi za wafanyakazi, ofisi za viongozi, kumbi za mikutano, zahanati, mabweni ya wanafunzi pamoja na jengo la huduma za jamii.

Mtaalamu wa Mazingira kutoka UDSM, Dk. Edmund Mabyuke, alisema chuo hicho kitatoa masomo mbalimbali ikiwamo ya utalii, biashara pamoja na ukalimu.

Diwani wa Kata ya Karabagaine ambapo chuo hicho kitajengwa alipongeza utaratibu unaoendelea dhidi ya ujenzi wa chuo hicho mkoani humo.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 9, 2023
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

**Dk. Mollel: Tunapiga vita ukoma kwa tiba bure kila tunakosikia ipo**


Ukurasa 13

**MUSWADA BIMA AFYA KWA WOTE**

Salamu na rai yake Rais mwaka jana, msimu wake sasa umetimu


Ukurasa 14

**IKIADHIMISHWA SIKU YA KIFAFA...**

**Bingwa Mshegenzi: Vyanzo vyake hivi, kuujua ugonjwa maabara kidogo sana**

# Samia alivyoufikia uamuzi mgumu, wanaonasa mimba kurudi darasani

• Wanaharakati; chereko na nderemo...

**Na Mwandishi Wetu**

SUALA la mimba na wanafunzi kukatishwa masomo imekuwa mada ngumu kitaifa. Hoja na misuguano ya haki kila kona hasa katika nafasi yao kushiriki imekuwa juu, wakiwamo wanaharakati binafsi.

Hadi anakasimiwa madaraka ya sasa, Rais Dk. Samia akitoka nafasi ya awali miaka miwili iliyopita, kutoka Makamu wa Rais nchini, ilikuwa marufuku kwa binti aliyepata mimba kurejea darasani.

Ni hali iliyochukua nafasi wakati huo, huku Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti ya ukaguzi wa hesabu wa miaka minne kati ya mwaka 2018 na 2021, akitumia vigezo vya halmashauri 27, amebaini idadi kubwa ya mabinti shule za msingi wanakatisha masomo kwa mimba.

Kwa mujibu wa CAG, hali ni mbaya zaidi ikiongozwa na Halmashauri ya Wilaya za Bunda (Mara), ikifuatiwa na Urambo (Tabora), kisha Tarime (Mara), huku Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ni kinara wa kunusuru wanafunzi wabaki masomoni kitaifa.

Mnamo mwaka 2019, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kushirikiana na kingine, Centre for Reproductive Rights, kiliwasilisha malalamiko kwa Kamati ya Wataalamu ya Haki na Ustawi wa Mtoto Afrika ((ACERWC)), kupinga kufukuzwa na kutengwa kwa wasichana wajawazito kutoka shule za umma nchini.



Samia Suluhu Hassan, akipokea tuzo yenye saini 50 za wanafunzi wa kike waliofaidika na Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF) katika hafla iliyofanyika, Zanzibar Juni, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho katika Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Fulgence Massawe, akihimiza haki ya wasichana wanaopata ujauzito kupata elimu na wanapaswa kuungwa mkono wasalie shuleni.

Pia, hata kabla ya hapo kwa miongo mingi, kumekuwapo nyendo za namna hiyo kusaka haki ya masomo kwa mwanafunzi anayeacha masomo

Mfano mojawapo ni mwaka 2013, asasi ya Centre for Reproductive Rights ilitoa chapisho inayoitwa 'Forced Out: Mandatory Pregnancy Testing and the Expulsion of Pregnant Students in Tanzanian,' mabinti wajawazito wakiangukia kwenye mimba.

Pia, kuna kesi zilizofunguliwa mahakamani na wanaharakati kutetea mabinti shuleni kuhusu hali hiyo, pasipo mafanikio.

**UAMUZI MGUMU**

Mnamo Novemba mwaka juzi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akatangaza rasmi uamuzi mgumu kuhusiana na hoja hiyo, sasa mabinti wanaopata mimba watawezeshwa kuendelea na masomo.

Salamu hizo zinazobeba mageuzi ya Rais Dk. Samia, katika miezi mitatu ya uongozi wake kitaifa, ilianza pale serikali ilipotangaza dhamira ya mageuzi kuwaruhusu wanafunzi waliokatiza masomo yao kwa sababu ya mimba, sasa wajiandae kurejea masomoni kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Ni hoja iliyoibua chereko kutoka kwa wanaharakati waliokuwa wakipaza sauti na kuishinikiza haki hiyo, sasa 'kufumba na kufumbua' imechukua nafasi yake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk, Leonard Akwilapo, akawaambia wakuu wa vyuo tajwa, akiwataka kuhakikisha wanafunzi wa

**INAENDELEA UK.12**

AFYA

# Samia alivyoufikia uamuzi mgumu, wanaonasa mimba kurudi darasani

INATOKA UK.11

kike walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, wawape fursa warudi darasani.

Akawaeleza wakuu wa vyuo hivyo, kutekeleza agizo hilo la kuwadahili wanafunzi hao kupitia alichotaja 'Mpango wa Elimu Haina Mwisho ifikapo Mwaka 2022.'

Pia, Dk. Leonard Akwilapo akavitaka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, viwe vimesajiliwa vituo vya kufanyia mitihani ya kidato cha pili na nne, kuwezesha kurejesha wanafunzi wa kike waliokatiza masomo.

Katibu Mkuu anafafanua: "Tulikuwa na mabishano mazungumzo marefu kwenye mpango wa kuimarisha na kuboresha elimu ya sekondari hapa nchini, moja ya makubaliano ilikuwa kutoa fursa kwa wasichana ambao wamekatiza masomo kwa njia yoyote ile.

"Wapate fursa ya kurudi na kuendelea na masomo. Tukasema tutatumia vyuo vya maendeleo ya wananchi, lazima tuanze hatuna uwanja, sio suala la kujadiliana, mambo mengine ya walimu mtatuachia sisi."

Kwa mujibu wa Dk. Akwilapo, wanafunzi hao watakaporejea masomoni ni katika vyuo 54, kuanzia mwaka 2022.



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**

### KUTOKA KWA WAZIRI

Akitangaza uamuzi wa maelekezo ya Rais Dk. Samia, waziri mwenye dhamana wakati huo miezi mitano baadaye, Novemba 24, 2021 jijini Dodoma, Prof. Joyce Ndalichako akasema wanafunzi wa shule za msingi na sekondari watakaokatisha masomo kutokana na sababu kama utoro, pia mimba watapewa fursa kurejea shule.

Waziri Prof. Ndalichako anatamka: "Leo natoa Waraka wa elimu ambao utaelezea ni lini wanafunzi watakaokatisha masomo kwa sababu ya mimba na changamoto nyingine watapaswa kurejea shuleni, leo leo natoa waraka hakuna kupoa zege halilali."

Anasema, serikali imefikia uamuzi huo kuwanusuru wapatao ujauzito watarudi darasani na kuendelea ma michakato ya kitaaluma kama walivyo wanafunzi.

### SAMIA AWAINUA

Pale inaporejewa madai mbalimbali ikiwamo angalizo la CAG na ustawi wa mabinti masomoni kwamba sababu kuu za kuacha shule kwa wasichana zilihusiana na ujauzito uliochangiwa na umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni, asili ya familia na masuala ya binafsi, rais akachukua hatua.

Katika uamuzi unaohusiana na mtazamo huo, Rais Samia, mbali na kuelekeza wanaojifungua kurejea masomoni, Desemba mwaka jana akaelekeza Sh. Milioni 960 zilizotengwa kwa ajili ya sherehe za Uhuru, zitumike kujenga mabweni ya shule nane za msingi, zenye wanafunzi walio na mahitaji maalum.

Hizo zinajumuisha Buhangija (Shinyanga), Goeko (Tabora), Darajani (Singida), Mtanga (Lindi), Songambele (Manyara), Msanzi (Rukwa), Idofi (Njombe), na Longido (Arusha).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu, George Simbachawene, katika hilo anafafanua kuwa shule hizo zimekwishagawiwa fedha za kujenga mazingira rafiki kuwakimu wanafunzi hao wenye mahitaji maalumu.

"Ikiwa ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwajali na kuwajengea mazingira rafiki watu wenye mahitaji maalum hapa nchini, hili ni jambo kubwa na la kishujaa na la kupongezwa sana," anasema.

Mnamo Oktoba mwaka jana katika azma ileile ya kujenga mazingira wezeshi kwa wanafunzi, Rais Dk. Samia akatoa Sh.bilioni mbili, kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa wilayani Arusha.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa hizo, kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu wanapata nafasi ya kuendelea na masomo.

## Dk. Mollel: Tunapiga vita ukoma kwa tiba bure kila tunakosikia ipo

**Na Yasmine Protace**

UKOMA si neno geni. Ni ugonjwa unaowapata baadhi ya watu, hata kuwasababishia wapoteze viungo vyao.

Kitaalamu inafafanuliwa kuwa ugonjwa wa kudumu unaosababishwa na bakteria.

Huwa, baada ya maambukizo kuna kipindi kati ya miaka mitano hadi 20 dalili hazionekani wala mtu kuzisikia. Pale dalili zinaonekana, huwa kwa mfumo wa kupumua, ngozi na macho.

Dalili zinapoanza kuonekana, mgonjwa hasikii tena, baridi, joto au maumivu. Kwa hiyo, hatambui kirahisi kuwa na jeraha, vidonda kuuma wala kufahamu uchafu na bakteria kuingia mwilini.

Mara zote, vidonda vinaweza kuwa vikubwa kwa sababu havitibiwi au vinachelewa kutibiwa. Ndiyo sababu wenye ukoma hupoteza viungo mwilini kama vile vidole mguuni, kutokana na majeraha yanayojirudia na kuugua muda mrefu.

Pia, kuna macho kutoona, kunakomuathiri mgonjwa. Imekuwa kawaida, baadhi ya familia zina wagonjwa wa ukoma na wanashindwa kuwapeleka hospitalini, hata kuwasababishia ulemavu wa viungo.

Katika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa ukoma, jamii sasa inatakiwa kutoa taarifa mapema, ili aliye mgonjwa atibiwe mapema.

Vilevile kwenye kinga, inashauriwa kupatikane elimu sahihi ya kukabiliana na ukoma, serikali ikibeba mikakati ya kuutokomeza ukoma. Tayari Wizara ya Afya, imebainisha stahiki itayosaidia katika kutokomeza ugonjwa ukoma nchini, ifikapo mwaka 2030.

Hapo inajumuisha kutoa mafunzo elekezi kwa watoa huduma hasa katika maeneo yenye wagonjwa, pia elimu kwa jamii juu ya ugonjwa huo.

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel anasema hayo jijini Dodoma katika tamko lake, Siku ya Ukoma Duniani akiwa na kaulimbiu "chukua hatua sasa, kutokomeza ukoma nchini."

"Serikali yetu imeendelea kuchukua hatua muhimu, ili kufikia malengo ya 'Utokomezaji Ukoma katika Taifa Letu' na tayari tumetengeneza mkakati wa kufikia visa sifuri vya Ukoma ifikapo mwaka 2030," anasema.

Anaongeza kwamba, kuna mkakati wa kutoa mafunzo elekezi kwa watoa huduma, hasa katika maeneo ambayo maradhi ukoma bado ni tatizo kwao.



Naibu Waziri Dk. Mollel anasema kupitia wataalamu katika maeneo ya kutoa huduma za ukoma, wizara inalenga kufanya uchunguzi katika kaya zote zenye wagonjwa, kuwabaini kuwaanzishia huduma mara moja wataogundulika kuugua.

Anaeleza kuwa, wizara inalenga kuongeza uwezo wa ufuatiliaji mwenendo wa ugonjwa ukoma katika vituo vyote vya kutoa huduma za afya nchini, ili kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Pia, Dk. Mollel ananena kwamba wizara inaendelea na juhudi kitafiti kuibua mbinu za kuharakisha kasi ya utokomezaji ugonjwa, kuona inaongezeka kwa kutambua mbinu mbalimbali za mapambano dhidi ya ukoma.

Hapo anawaelekeza Waganga Wakuu wa Halmashauri, kuhakikisha wanajumuisha shughuli za kutokomeza ukoma, sambamba na mikakati ya afya katika maeneo yao ya kazi.

Rai yake ni kwa mamalaka za mikoa kuhakikisha kila mgonjwa anayeibuliwa, anatambuliwa makazi yake, kijiji na kata anakotoka, iwe ndani au nje ya wilaya, hata mkoa.

Msisitizo wa waziri ni kwamba, kama mgonjwa atatokea nje ya mkoa husika, inapaswa kuhakikishwe taarifa zake zinapelekwa alikotoka, ili kusaidia ufuatiliaji na uchunguzi wa maambukizi, hata kuwezesha tiba na kinga ya maradhi husika.

Dk. Mollel anaagiza kwamba kila halmashauri kuhakikisha wanafuatilia mwenendo wa ukoma katika ukanda wao, wanakuwa na takwimu sahihi za wagonjwa kulingana na maeneo,vijiji au mitaa wanakopatikana.

AFYA

## MUSWADA BIMA AFYA KWA WOTE UKIWA MEZANI

# Salamu na rai yake Rais mwaka jana, msimu wake sasa umetimu

**Na Mwandishi Wetu**

MUSWADA wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote uko mezani kuwasilishwa kwa mara ya pili kwenye kikao cha Bunge kinachoendelea jijini Dodoma. Matarajio ya kujadiliwa na kupitishwa, utekelezaji wake kuanza Julai Mosi mwaka huu. Ni taarifa ya neema kiafya kwa Watanzania wote.

Katika rai yake kwa umma mwaka jana, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwasilisha hoja akatamka: "Niwaombe tutakapopitisha sheria hii Watanzania tukajiunge na mifuko ya bima."

Ni kauli ya Dk. Samia akiwa kwenye mkutano na viongozi wa dini katika maadhimisho ya Jubilee ya Miaka 50 ya Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) mjini Dodoma.

Rais akabainisha kwamba, anaufahamu udhaifu uliopo kwenye mifuko ya bima na hatua zinazochukuliwa, hivyo akaahidi na kutoa rai kwamba, itakapoanzishwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, itakuwa madhubuti, pamoja na kanuni zitakazowezesha watu wote kutibiwa kwa ufanisi.

"Mfuko huu utahakikisha mtu anapata matibabu yote anayopaswa kupata. Huu ni kama upatu ambao Watanzania wote tunakwenda kucheza na kati yetu atakayepatwa na shida, upatu huo unamsaidia," akatamka.

Rais Dk. Samia akaendelea:"Ni kupitia Bima ya Afya kwa Wote ndipo tutaweza kutoa matibabu kwa kila Mtanzania anayeishi ndani ya nchi yetu.

Kimsingi, ni nukuu nzito kwa kiongozi mkuu wa nchi, kwa namna alivyojipanga na serikali yake kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za matibabu.

Ikirejewa tamko hilo la mkuu wa nchi, inahamasisha umuhimu wa kila Mtanzania kujiunga na bima hiyo, kwani inaelezwa ugonjwa hauchagui umri, siku na wakati na bima ndiyo mwokozi wakati wowote.

Hadi sasa serikali iliyopo madarakani inaendelea na uwekezaji wa mahitaji ya miundombinu katika matibabu, katika maeneo mbalimbali nchini, ikisimamiwa kwa karibu na mwongozo wa kisera na Mpango wa Taifa wa Afya ya Msingi (MAM), wenye miaka 15 sasa.

Ikirejewa takwimu ni kwamba, hadi sasa asilimia 85 ya Watanzania hawana bima za afya, huku kukishuhudiwa matukio ya baadhi ya kaya zinazoelemewa na mahitaji ya kitabibu, kulazimika kuuza rasilimali zake, kupata fedha za kugharamia tiba.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa kwenye Mkutano wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) jijini Dodoma mwaka jana, ambako akatangaza ujio wa muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, akidokeza sura na manufaa yake. **PICHA: MTANDAO**

> **Mfuko huu utahakikisha mtu anapata matibabu yote anayopaswa kupata. Huu ni kama upatu ambao Watanzania wote tunakwenda kucheza na kati yetu atakayepatwa na shida, upatu huo unamsaidia.**

Tafsiri ya Bima ya Afya kwa Wote, msingi wake ni utaratibu wa kuwezesha wananchi kupata huduma za matibabu kwa urahisi bila kikwazo cha fedha kwa kuchangia huduma hizo kabla ya kuugua.

Hivyo, basi dhana ya bima ya afya inajengwa katika misingi ya mshikamano wa kijamii katika kugharamia huduma za matibabu kwa makundi na hata atakapougua, anapata huduma bila ya kikwazo cha fedha.

**MCHAKATO ULIKOTOKA**

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya Maandalizi ya Kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote yalianza tangu mwaka 2012 na kutokana na umuhimu wake, ilizimika kuchukua muda mrefu kuiandaa.

Ni hali inayotokea, huku kukishuhudiwa ongezeko la magonjwa na hasa yasiyoambukiza, ikiendana na gharama kubwa ya matibau. Inarejewa mfano wa magonjwa kama saratani, figo na moyo yako juu.

Kutokana na gharama kubwa za matibabu, baadhi ya wananchi wanashindwa kuzimudu na kupata athari za kiafya na wakati mwingine, hata kupoteza maisha kwa kukosa huduma bora za afya.

Ili kutatua changamoto hiyo, serikali ikadhamiria kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ili kuimarisha mfumo wake kwa kuwezesha wananchi kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua kwa kupitia bima, kuwawezesha kupata huduma bora za afya wakati wote wanapozihitaji karibu na maeneo wanakoishi.

Bado kumekuwapo magumu kwenye mifumo ya kugharamia, kama vile wananchi kukosa fedha za matibabu ya papo kwa hapo, idadi ndogo ya wananchi kujiunga na bima na hiari ambayo imesababisha wengi kujiunga na bima wakiwa wagonjwa.

Chimbuko la kuandaliwa kwa muswada huo, ni kutimiza wajibu wa serikali kikatiba wa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya pasipo kikwazo.

Sheria iliyopo inaweka hiari wa umma katika kujiunga na bima ya afya, hatua inayotajwa kusababisha wengi kujiunga wakiwa tayari na matatizo ya kiafya.

**MANUFAA YA BIMA**

Yapo manufaa ambayo wananchi wamekuwa wakiyapata na watayapata , endapo sheria hiyo itapitishwa na bunge na kuanza kutekelezwa, kwa kundi kubwa la wananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila ya kikwazo cha fedha.

Wizara ya Afya katika taarifa yake inahimiza kuwapo ustahimilivu wa mfuko huo katika kutoa huduma, kwa sababu wengi watachangia na sio wote wataugua; pia kutakuwapo uboreshaji huduma katika vituo vya kutoa huduma za afya vya umma.

Hapo panatajwa kuimarika upatikanaji dawa na vifaa tiba, kuanzia zahanati hadi hospitali ngazi ya taifa; kuna kuimarika usimamizi na udhibiti katika utoaji wa huduma kwenye mfuko wa bima za afya wa umma na binafsi.

Manufaa mengine yanatajwa ni kuimarishwa hali ya kipato kwa wananchi na kuwaondolea umasikini wananchi kutokana na gharama kubwa za matibabu na kuwawezesha kupanga mipango ya maendeleo.

**SURA YA MUSWADA**

Kupitishwa muswada huo, utawagusa zaidi walioko kwenye sekta binafsi na waliojiajiri, ikiwamo mashambani waliko Watanzania wengi zaidi.

"Watu walio katika sekta isiyo rasmi watajiunga kwa kaya au mtu mmoja mmoja, kaya itakuwa na watu sita, akiwamo mchangiaji na mwenza mmoja, pamoja na wategemezi wengine wanne.

"Wategemezi wa mchangiaji wanaweza kuwa baba, mama, wakwe, watoto wa kuzaa na kambo na ndugu wa damu mwenye umri usiozidi miaka 21. Kaya yenye wategemezi zaidi ya wanne itakuwa na fursa ya kuanzisha kaya nyingine," inafafanua Wizara ya Afya, katika dodoso lake la maudhui ya muswada.

Inaelezwa, wanaojiunga na bima ya Afya kwa Wote, watanufaika na huduma ikiitwa "Kitita cha Mafao ya Huduma Muhimu (Standard Benefit Package)" na kila skimu ya bima ya afya italazimika kuitoa, ikiwa ni haki ya kila mwanachama.

Kitita hicho kinatajwa kuzingatia huduma zote zilizopo katika mwongozo wa tiba, Orodha ya Taifa ya Dawa Muhimu (NEMLIT) na aina ya magonjwa kama ilivyoainishwa katika Miongozo ya Tiba ya Kimataifa.

Hapo kuna mambo kama vile: Ada ya uandikishaji na kumuona daktari; gharama za vipimo; dawa aina zote (NEMLIT); upasuaji mdogo na mkubwa; kulazwa; afya ya kinywa na meno, matibabu ya macho; vifaa saidizi (l na mazoezi ya viungo (physiotherapy), huduma zikipatikana kuanzia ngazi ya zahanati, hospitali maalum hadi Hospitali ya Taifa na vituo vya umma, pia binafsi vilivyosajiliwa na skimu husika nchi nzima.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, bima za afya, zitasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) itakayokuwa na jukumu la kuhakikisha kila skimu inatimiza vigezo na wanachama watakuwa na nafasi ya kutoa malalamiko wanapoona hawaridhishwi na huduma.

AFYA

KESHO IKIADHIMISHWA KIMATAIFA SIKU YA KIFAFA...

# Bingwa Mshegenzi: Vyanzo vyake hivi, kuujua ugonjwa maabara kidogo sana

**Na Christina Mwakangale**

NI darasa la afya linalotaka utulivu. Inaelezwa kwamba, mfumo wa umeme kwenye ubongo wa binadamu, mara tu ukipata tatizo, huwa kuna sababu ambazo, mojawapo ni sehemu inapokatiza mfumo huo, ama pana uvimbe au kovu.

Ajali ya aina yeyote, ikiwamo barabarani, ambazo kwa mtazamo wa nje athari zake hazibainiki moja kwa moja, huweza kuathiri mfumo wa umeme wa ubongo na mawasiliano, kisha mtu anapoteza au kutopoteza fahamu.

Bingwa wa tiba magonjwa ya mfumo wa fahamu, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila, Dk. Brighton Mshengezi, anafafanua hayo katika mazungumzo na Nipashe, kuhusu kiini cha ugonjwa kifafa.

Maradhi kifafa duniani huadhimishwa kila wiki ya pili ya mwezi Februari. Nchini Tanzania, siku hiyo inatumika kutoa elimu kwa umma, nchini ikiadhimishwa kesho, Ijumaa.

Bingwa huyo anaeleza namna ugonjwa huo ulivyo na tafsiri yake, ikiwa na taswira tofauti na wakati mwingine ili kuubaini hautegemei vipimo vya kisayansi, bali mahojiano binafsi kati ya mgonjwa na mtaalamu tiba.

"Kwa mfano mtu anayeugua malaria, au presha atakuja hapa utamfanyia vipimo, vitakujibu hapo hapo anaumwa. Ila mgonjwa wa kifafa, anaweza kuja na jamaa au mwenyewe na mwonekano wake ni mzima tu.

"Ila pale unapouliza sababu yao kufika hospitali, jamaa atakwambia huyu ndugu yangu huanguka, hupoteza fahamu, mkono au mguu hukakamaa kwa muda fulani, au mgonjwa mwenyewe akasema, hafamu kinachomtokea, ila anasimuliwa," anasema.

Anaendelea:"Ugonjwa huu naweza kusema unategemea zaidi mazungumzo kwa asilimia 80 na vipimo vitamaliza kiwango, tofauti na mtu mwenye VVU (Virusi vya Ukimwi), malaria kipimo kitaonyesha moja kwa moja ana maambukizi," anafafanua.

**VYANZO VYAKE**

Bingwa huyo Dk. Brighton Mshengezi, anasema, sababu ya kuadhimisha siku hiyo kesho, ni kukuza elimu kwa umma kwamba ni miongoni mwa magonjwa yenye utata.

"Wapo wanaoamini unaambukizwa na mtu anayeugua, wanamtenga, wanasema ukikoholewa na mwenye kifafa umepata, watu wengi hawaendi hospitali wanadai ni kurogwa," anasema Dk. Mshengezi.



Tabibu bingwa wa magonjwa ya mfumo wa fahamu kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Brighton Mshengezi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **Ni kama umeme wa nyumbani ikitokea hitilafu umeme utakatika, pia umeme kwenye ubongo usiporekebishwa kuna athari, hata kifo.**

Anafafanua kwamba ugonjwa huo, pia unatambuliwa na wataalamu wa Chama cha Kudhibiti Kifafa Tanzania (TEA), yeye akiwa mwanachama, yapo wanayoyajadili ikiwamo kutafiti na kuja na suluhisho au mapendekezo.

Bingwa Mshengezi anataja sababu mbili zinazojulikana na zisizojulikana, akirejea athari ni kwenye umeme wa ubongo unapopata hitilafu.

Anasema, chanzo kinaweza kuwa kovu kwenye ubongo kusababishwa na ajali kichwani, mtoto aliyevutwa wakati wa kuzaliwa, au uvimbe hasa kwa wanaougua saratani.

"Mtu anaweza kuwa na dalili ya kukakamaa, apoteze fahamu au asipoteze fahamu. Si kifafa chote unapoteza fahamu, mwingine anayeugua anakusimulia mwenyewe ambacho kinamkumba kwa sekunde au dakika chache," anasema.

**INATOKEAJE?**

Bingwa huyo anaeleza kwamba mtu anatokewa na maradhi kifafa kazini, akicheza, usingizini na akiamka anajikuta mwili, mgongo, viungo vimechoka, kifafa kilimpitia usingizini na mfumo wa umeme ukikatizwa kila mara na inaweza kuleta kifo."

"Nilipokuwa nasoma shule ya Jumapili (Sunday School), mtoto mwenzangu tukiwa tunaimba akakaa kimya kwa muda mfupi bila ya kufanya chochote, amezubaa, nilimtania sikujua. Baada ya kuwa 'neurologist' (bingwa mishipa ya fahamu) nimebaini mtoto huyu kumbe aliugua," anaeleza bingwa huyo

Dk. Mshengezi anaeleza kwamba kuna wakati huwa sababu pia maambukizi ya minyoo itokanayo na nyama ya nguruwe, ambayo haikuandaliwa vyema, husababisha tatizo hilo.

Kadhalika, anasema mama anapojifungua mtoto akavutwa kwa kutumia vyuma, mfumo wa umeme unaweza kusumbuliwa na kuwa chanzo cha kifafa wakati akikua au ukubwani.

"Uzuri mtoto akipata uvimbe au tatizo utotoni, linaweza jirekebisha kwa kuwa anakua. Ila tatizo kujitokeza ukubwani utashangaa mbona hakuumwa akiwa mtoto," anafafanua.

**DEGEDEGE VS KIFAFA**

Bingwa huyo anasema jamii imejihusisha sana na kifafa, pia degedege, akitaja baadhi ya viashiria vinafanana, hakuna uhusiano kati yao.

"Degedege ni tukio la mtu hupoteza fahamu awe mtoto au mtu mzima. Lakini, degedege ni tukio litokanalo na sababu, aidha anaumwa, mtu hajala chakula, sukari imeshuka mwilini au mgonjwa wa kisukari kazidisha dawa.

"Watu bado hawaamini kwamba degedege huweza kumpata hata mtu mzima, si mtoto tu. Kifafa ni ugonjwa na degedege ni tukio la sababu fulani, ila hata mtu mwenye kiharusi anaweza kupata degedege," anafafanua bingwa huyo.

Daktari huyo anaiambia Nipashe kuwa, kifafa hakina umri, yeyote huugua na unatibika baada ya historia ya mgonjwa, kipimo cha MRI kubainisha matokeo sahihi.

"Imebainika kwa asilimia 70 waliotumia dawa kwa ufasaha na kwa kufuata dozi ambayo kwa kawaida ni tiba ya miaka mitatu hupona kabisa. Hiyo asilimia 30 ndio wale wasiofuata masharti. Dawa anazitumia, mgonjwa huenda kuirekebisha mfumo wa umeme kwenye ubongo.

"Ingawa kipimo kikionyesha tiba ifaayo ni upasuaji, hufanyiwa upasuaji wa ubongo ili kuirekebisha, kuondoka sehemu iliyo na hitilafu.

"Ni kama umeme wa nyumbani ikitokea hitilafu umeme utakatika, pia umeme kwenye ubongo usiporekebishwa kuna athari, hata kifo," anasema bingwa huyo.

**ATHARI ZAKE**

Dk. Mshengezi anaeleza kuwa zipo athari kama za ajali aina tofauti, mathalan kuathirika na moto jirani au barabarani.

"Kuna mtu utakuta anakuja hapa anasema yeye ni dereva, na udereva ndio kila kitu yaani maisha yake, anaenda safari masafa marefu umpe dawa aendelee na kazi. Ingawa mgonjwa huyo huyo wa kifafa asipopata mapumziko, usingizi wa kutosha ni hatari kwake.

"Kwa kifupi, mtu huyo anajiongezea kupata degedege kwenye kifafa. Mwingine atakwambia, anashangaa alijikuta gari ipo kwenye mtaro, hajui ilikuwaje," anaeleza, huku akihitimisha kwa takwimu za duniani kwamba, wapo wagonjwa wanaougua kifafa milioni 67.



# Exim yahitimisha kampeni utoaji madawati shule za msingi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Exim imehitimisha kampeni ya kugawa madawati katika shule za msingi nchini katika Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma.

Kampeni hiyo ililenga kugawa madawati 1,000 imehitimishwa kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Chemba kwa kupatiwa madawati 150.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa mwaka 2021 na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwa benki hiyo.

Akipokea madawati hayo shuleni hapo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliipongeza benki hiyo kwa kutambua matatizo wanayokumbana nayo wanafunzi na kuamua kuwasaidia kupata samani muhimu.

Alisema kilichofanywa na benki hiyo ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuboresha hali ya utoaji wa elimu bora nchini kwa kukabiliana na tatizo kubwa la uhaba wa madawati.

"Niwapongeze sana Benki ya Exim kwa kampeni hii iliyogusa maelfu ya wanafunzi katika mikoa yote ambayo imefikiwa na kampeni hii. Alama mliyoiacha itadumu kwenye mioyo ya watoto hawa kwa muda mrefu na zaidi pia imesaidia jitihada za serikali kuhakikisha kila mwanafunzi anakaa kwenye dawati," alisema.

Aidha, aliiomba benki hiyo kuangalia namna ya kumalizia tatizo la uhaba wa madawati 86 iliyobaki shuleni hapo, huku akitoa wito kwa halmashauri kuhakikisha zinashiriki kikamilifu kumaliza changamoto zilizoko kwenye sekta ya elimu mkoani humo.

Kwa mujibu wa Senyamule, baadhi ya changamoto zilizoko ni uhaba wa vyumba vya madarasa, madawati na matundu ya vyoo badala ya kusubiri msaada wa serikali kwa kuwa pia wanawajibu wa kuisaidia serikali kuboresha hali ya upatikanaji wa elimu nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Gerald Mongella, alisema kuna shule 110 huku uhaba wa madawati ukiwa ni 9,011 na kwamba Shule ya Msingi Chemba ina uhitaji wa madawati 236, hivyo msaada wa madawati 150 uliotolewa na Benki ya Exim unaifanya shule hiyo ibakiwe na upungufu wa madawati 86.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, aliahidi kumaliza upungufu huo uliobakia na kwamba walichagua Mkoa wa Dodoma kuhitimisha kampeni hiyo kutokana na heshima ya mkoa huo wenye hadhi ya makao makuu ya serikali.

Aliitaja mikoa mingine iliyonufaika na kampeni hiyo kuwa ni Dodoma, Mwanza, Lindi, Mbeya, Mtwara, Tabora, Shinyanga na Tanga.

# Uongozi Bonde la Wami wakemea uchimbaji holela visima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UONGOZI wa Bonde la Maji la Wami-Ruvu umekemea tabia ya uchimbaji holela wa visima vya maji bila kibali, huku mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ikitajwa kuwa vinara wa uchimbaji huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo kuhusu utekelezaji wa shughuli za bonde hiyo, Mkurugenzi wa Bonde hilo, Mhandisi Elibariki Mmassy, alisema kwa sasa kumeibuka tabia ya uchimbaji wa visima holela huku kukiwa hakuna mfumo mzuri wa utoaji majitaka hali inayohatarisha afya za watumiaji bila kujua. Alisema: "Jiji la Dodoma kabla ya serikali kuanza kuhamia huku ongezeko la visima holela lilikuwa visima 50-40 kwa mwezi kwa sasa imeenda mara mbili au mara tatu hasa kipindi cha ukame kumekuwa na ongezeko la visima holela."

Mkurugenzi huyo alisema kwa Dar es Salaam tatizo hilo ni kubwa kwamba vilichimbwa visima 300 hasa kipindi cha ukame na wameendelea kukabiliana na tatizo hilo kwa kuwatambua waliochimbiwa ili kuangalia ubora.

Alifafanua kuwa visima hivyo vinachimbwa bila utaratibu na wamekuwa wakiwakamata na kuwachukulia hatua.

Alisema kwa Mkoa wa Morogoro wamekuwa wakifuata taratibu kutokana na maeneo mengi kuwa yenye chumvi.

"Ni kosa kisheria kuchimba kisima bila kuwa na kibali, faida ya kuwa na kibali ni kwamba ukishaomba tunakagua eneo kama linafaa kwa ajili ya uchimbaji wa kisima."

"Hazina ya maji iliyoko chini ya ardhi mtu mmoja akiamua kuichafua anachafua kiwango kikubwa cha hazina iliyoko, kama mnavyoouona Mji wa Dodoma ulivyomkubwa lakini unategemea hazina ya maji kutoka Makutupora,"alisema.

Alisema ni vigumu kusafisha maji yaliyochafuka chini ya ardhi hivyo ni muhimu kwa wanaohitaji kuchimba kisima kuomba kibali ili eneo husika likaguliwe na kupata ushauri.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, bonde hilo limejipanga kuwa na mabwawa yanayohifadhi maji.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa tatu kulia), akipokea msaada wa madawati 150 kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu kwa ajili ya Shule ya Msingi Chemba, wilayani Chemba, mkoani humo juzi, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa madawati unaoikabili shule hiyo. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Gerald Mongella (wa pili kulia) na viongozi waandamizi wa wilaya hiyo pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali: Idadi vifo vya watoto mwaka jana ilipungua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa mwaka 2022 kimepungua hadi vifo 43 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai ukilinganisha na vifo 67 ilivyokuwa mwaka 2015/16.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa matokeo muhimu ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria Tanzania wa mwaka 2022.

"Haya ni matokeo makubwa ya juhudi zinafanywa na serikali katika utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea katika mpango wetu wa tatu wa maendeleo wa taifa ambao unalenga kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano hadi vifo 40 katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai ifikapo mwaka 2025/26."

Kadhalika alisema hali hiyo inachangiwa na juhudi za serikali za kuhakikisha utekelezaji wa bima ya afya kwa wote, ambapo kwa sasa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka ya mwaka 2022, yanaonesha kuwa asilimia 6.2 ya Watanzania wote wana bima ya afya.

Alisema kati ya idadi hiyo wanawake wakiwa ni asilimia 6.3 na wanaume ni asilimia 6.1.

Aidha, alisema matokeo ya utafiti wa mwaka 2022 yanaonesha kuwa asilimia 2.7 ya watoto wana uzito pungufu kulinganisha na kilichofanyika mwaka 2015/16.

Alisema vilevile asilimia 12 ya watoto chini ya miaka mitano kwa mwaka 2022 wana uzito pungufu ikilinganishwa na asilimia 14 katika utafiti uliofanyika mwaka 2015/16. Ummy alisema mikoa ambayo inaongoza kwa udumavu mkali ni Rukwa asilimia 20.7, Njombe asilimia 18.5 na Iringa asilimia 17.3.



# Mwalimu azua taharuki akisambaza picha mitandao kijamii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWALIMU wa kujitolea katika Shule ya Sekondari Sinde ya jijini Mbeya, Evarist Chonya, amezua taharuki baada ya kusambaza mitandaoni picha zikionyesha baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakiwa wanasoma huku wamekaa chini.

Picha hizo zilisambaa juzi kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii, huku ikielezwa kuwa wanafunzi hao wanakaa chini kutokana na uhaba wa madawati unaoikabili shule hiyo jambo ambalo liliibua taharuki miongoni mwa viongozi wa serikali.

Baada ya kupata taarifa hiyo, baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya pamoja na maofisa mbalimbali wa Idara ya Elimu mkoani Mbeya, walifika katika shule hiyo kwa ajili ya kuangalia hali ilivyo na kubaini kuwa taarifa hizo hazina ukweli wowote.

Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Anathalia Luwungo, alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,300 kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne ambao wote wanakaa kwenye madawati na hakuna mwanafunzi hata mmoja ambaye anakaa chini kama ambavyo picha hizo zilikuwa zinaeleza.

Alisema mwishoni mwa wiki waliyatoa madawati yote nje ya vyumba kwa ajili ya kuyaandika majina ya wanafunzi ili kila mwanafunzi awe na dawati lake ambalo atakuwa analitumia na kulitunza mpaka atakapohitimu kidato cha nne.

Alisema wakati shughuli hiyo ikiendelea mwalimu huyo aliwarejesha darasani baadhi ya wanafunzi na kuwaamuru wakae chini kisha akawapiga picha kwa nia ambayo haijulikani.

"Sisi hapa tuna madawati mpaka ya ziada, sasa tulipomhoji kwanini aliwarejesha wanafunzi darasani wakati madawati yako nje akajibu kwamba muda wa kipindi chake ulikuwa umefika na hivyo alitaka awafundishe," alisema Mwalimu Luwungo.

Aliwatoa wasiwasi wazazi na walezi wa watoto wanaosoma kwenye shule hiyo kuwa hakuna tatizo la uhaba wa miundombinu ya aina yoyote ikiwamo madawati.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga, alisema mwalimu huyo ameshachukuliwa hatua za kusimamishwa kazi na kwamba kwa sababu siyo mwajiriwa wa serikali atafukuzwa kabisa kwenye kazi hiyo.

Alisema mbali na kumfukuza kazi pia wametoa taarifa Jeshi la Polisi ili achukuliwe hatua zaidi kwa kosa la kusambaza taarifa za uongo ambazo zimezua taharuki kwenye jamii.

Kisiga alisema shule zimekuwa na utaratibu wa kuwaruhusu walimu wa kujitolea kufanya kazi kwenye shule zao endapo wana uhaba wa walimu na kwamba wamekuwa wakiwatumia walimu hao baada ya kujiridhisha.

"Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuboresha miundombinu ya shule zetu, kwenye jiji letu hatuna tatizo la uhaba wa madawati kwa hiyo tumeshatoa taarifa polisi ili kijana huyu achukuliwe hatua kwa kutoa taarifa za uongo," alisema Kisiga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka walimu kuacha kutumiwa vibaya na wanasiasa na badala yake wafanye kazi kwa kushirikiana na serikali kama ambavyo wanakuwa wameaminiwa.

Alisema ili kukomesha tabia hizo wameshaanza kuchukua hatua dhidi ya mwalimu huyo ambapo hakuziweka wazi hatua hizo kwa maelezo kuwa jambo hilo liko kwenye hatua za uchunguzi. Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema mkoa huo hauna shida ya madawati kama ambavyo picha zilizokuwa zinasambaa zilikuwa zinatafsiriwa.



Lori la mizigo likiwa limeanguka na kufunga barabara kuu ya Tanzania na Zambia kwa zaidi ya saa mbili, eneo la mteremko wa Iwambi jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sheria ndogo za halmashauri chanzo upotevu mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHERIA ndogo za Halmashauri ya Jiji la Mbeya zinazosimamia ukusanyaji wa ushuru, zimetajwa kuwa chanzo cha upotevu wa mapato kutokana na wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru huo.

Aidha sheria hizo zimedaiwa kuwa chanzo cha baadhi ya maofisa wa Jiji hilo kushirikiana na wafanyabiashara kuhujumu ukusanyaji wa mapato kwa kufanya mazungumzo ya siri yanayowafanya wasilipe ushuru wanaostahili.

Hujuma zinazosababishwa na sheria hizo, iliibuliwa juzi na baadhi ya madiwani kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo kilichokuwa na lengo la kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 na kupitisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2023/2024.

Diwani wa Kata ya Sinde, Fanuel Kyanula, alisema sheria hiyo ndogo inaeleza kuwa halmashauri inatakiwa kukusanya ushuru usiozidi asilimia 0.3 na kwamba zaidi ya hapo inatakiwa kufanyika mazungumzo kati ya mfanyabiashara na halmashauri.

Alisema kipengele hicho cha sheria kinachochea baadhi ya wafanyabiashara kutolipa ushuru na wengine kufanya mazungumzo na maofisa wa Jiji wasiokuwa waaminifu ili wasilipe ushuru kwa kuwapa chochote.

"Tunapoteza fedha nyingi sana kupitia kipengele hiki, wapo wafanyabiashara ambao kwa kupitia kipengele hiki wanakwepa kabisa kulipa ushuru na wengine wanatupiga kwa kufanya mazungumzo na maofisa wetu wasiokuwa waadilifu," alisema Kyanula. Alishauri halmashauri hiyo kufanya mikutano ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara ili kuwapa elimu ya umuhimu wa kulipa ushuru wa huduma mbalimbali wanazotoa.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga, alisema alikiri kuwapo kwa tatizo hilo lakini akaeleza kuwa tayari walishaanza kuchukua hatua ya kudhibiti mianya hiyo ya upotevu wa mapato.

Alisema tatizo hilo lilikuwa kubwa zaidi kwa miaka iliyopita lakini kwa sasa limedhibitiwa kwa kiasi kikubwa jambo ambalo limesaidia hata ukusanyaji wa mapato kuongezeka.

Alisema baada ya kuziba mianya hiyo, mpaka sasa halmashauri hiyo imefikia asilimia 66 ya ukusanyaji wa mapato wakati mwaka uliopita wa fedha kipindi kama hiki walikuwa hawajafikia kiwango hicho.

Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh DorMohamed Issa, alisema mpaka kufikia Februari 3, 2023 halmashauri hiyo ilikuwa imefikia asilimia 64.3 ya malengo ya makusanyo wakati awali walikadiria kufikia asilimia 59.

Alisema hali hiyo ya makusanyo inaleta matumaini na ana uhakika mipango inayopangwa na halmashauri hiyo itatekelezwa kama ambavyo imekusudiwa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka madiwani hao kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wa bajeti hiyo ili kuwaletea wananchi maendeleo yanayokusudiwa.

# Wananchi wanadaiwa kuua wanyama Hifadhi ya Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya wananchi waliobaki kwenye vijiji vilivyoondolewa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, wanadaiwa kuanza kufanya vitendo vya ujangili ndani ya hifadhi hiyo kwa kuwaua wanyama.

Hivi karibu serikali ilipitia upya mipaka ya hifadhi hiyo na vijiji kwa kufanya marekebisho ya mipaka iliyokuwa inatafsiriwa kwenye Tangazo la Serikali namba 28 (GN.28) ya mwaka 2008 ambapo vijiji vitano kati ya 39 viliondolewa kabisa kwenye hifadhi hiyo.

Hata hivyo wananchi hao waliachwa kwa muda ili waendelee kuyahudumia mazao ambayo walikuwa wameshayapanda ili wakivuna ndio waondoke lakini wanadaiwa kuanza kufanya vitendo vya uhalifu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema Februari 8, mwaka huu mtu mmoja aitwaye Michael Mwambaja mkazi wa Kijiji cha Mdundasi kilichoko katika Kata ya Luhanga alikamatwa akiwa amemuua twiga kwa lengo la kupata kitoweo.

Alisema mtu huyo alikuwa na mwenzake ambaye alikimbia baada ya tukio hilo na kutokomea kusikojulikana na kwamba huruma ya serikali imeanza kuwa tatizo kwenye hifadhi.

"Naviomba sana vyombo vya dola vitusaidie kushughulika na hawa watu, huyu ameua twiga tunaomba akifika mahakamani haki ikatendeke ili kama mtu huyu atakuwa na haki aipate na kama serikali ndio ina haki iipate," alisema Homera.

Alisema mbali na kumkamata mtu huyo, pia hivi karibuni watu wengine walinaswa na meno ya tembo katika Wilaya za Chunya na Kyela wakisafirisha meno ya tembo.

Alisema katika Wilaya ya Chunya walikamata meno 35 na Kyela walikamata meno 38 jambo ambalo linaashiria kwamba vitendo vya ujangili vinaendelea kwenye hifadhi mbalimbali za taifa.



# Walimu watakiwa kukaa mguu sawa ujio mitaala mipya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WALIMU wa shule za msingi Zanzibar wametakiwa kujiweka tayari kwenda sambamba na mitaala mipya itakayotumiwa kwa shule hizo ambayo imelenga kuwapo kwa ubora wa elimu nchini na ufaulu wake.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, wakati aliposhiriki katika mafunzo ya walimu wa msingi kuhusu matumizi ya mitaala mipya ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo inatarajiwa kuanza mwaka huu.

Alisema mitaala mipya imejikita katika ubora wa elimu ambayo imeweka msingi katika ufaulu kwa mitihani ya taifa.

Aidha alifahamisha kuwapo kwa mitaala hiyo kumekuja baada ya malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa sekta ya elimu kuhusu kufanyika kwa maboresho ya mitaala ya elimu ya msingi.

"Huo ndiyo ujumbe wangu kwa walimu wa shule za msingi kuhakikisha kwamba tunajipanga kwa ajili ya kutekeleza mitaala ya elimu ya msingi ambapo matarajio yetu kuona kwamba tunapata ufaulu mzuri wa mitihani ya taifa," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, Abdalla Mohamed Mussa, alisema mtaala mpya wa elimu kwa shule za msingi umekidhi mahitaji yote ikiwamo kuwapo kwa masomo wastani kwa wanafunzi hao.

"Mtaala wa elimu ya msingi unakwenda na mahitaji ya wanafunzi wa shule za msingi hatua ambayo itaongeza ufaulu wa wanafunzi kwenda sekondari," alisema.

Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi, Fatma Maulid Ramadhan, alisema matarajio makubwa ya wizara ni kuona walimu wanaongeza juhudi ambazo matokeo yake ni kuwapo kwa ufaulu utakaoridhisha kwenda sekondari.

Mkaguzi wa Elimu Sekondari, Maimuna Fadhil Abasi, akizungumza na walimu wa Michakaeni Pemba aliwataka kujituma na kufahamu kwamba wamekabidhiwa jukumu kubwa la kufundisha wanafunzi na kuona wanafikia viwango vya kuingiza elimu ya juu.



Mwanasheria wa Shirika la Magazeti Zanzibar na mwandishi wa habari mwandamizi, Juma Khamis, akichangia mada wakati wa mafunzo ya kupitia sheria kandamizi za uandishi wa habari yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar, kwa kushirikiana na Shirika la Internews eneo la Tunguu, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Masheha watakiwa kuorodhesha maeneo ya uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, amewataka masheha kuorodhesha maeneo yote ya uwekezaji ambayo hayatumiki ili kuyatambua na kuwapatia wawekezaji wingine kuwekeza miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana Zanzibar wakati akizungumza na masheha, kikao ambacho kilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa pamoja na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maji na Maliasili.

Alisema yapo maeneo mengi ya ardhi wamepewa wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza miradi mbalimbali lakini hadi sasa hayajatumiwa kikamilifu, huku wakiwamo wawekezaji wengine wakitaka kuwekeza.

Alisema masheha ndio wanaoyatambua maeneo hayo, kwamba wanatakiwa kuyatambua na kuyawasilisha serikalini kwa ajili ya matumizi mingine.

"Wizara ya Ardhi tumeanza kuyatambua kwa kuyaorodhesha maeneo ya ardhi ambayo wamepewa wawekezaji lakini kwa bahati mbaya hayajaendelezwa kwa shughuli zilizokusudiwa," alisema.

Masheha hao walisema kuwa watayafanyia kazi yaliyotakiwa kuorodhesha maeneo hayo ambayo yapo kwa baadhi ya maeneo bila ya shughuli za uwekezaji.

# Kiongozi CCM akerwa na kauli za wanasiasa kuhusu utengano

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohammed Said Dimwa, amekemea kauli zisizofaa za kuhubiri utengano, upotoshaji na kubeza zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa kuhusu maendeleo yanayopatikana chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Alisema wanasiasa hao wanatakiwa kujitathmini juu ya mwenendo wao unaolenga kuchafua thamani, tija na mafanikio yaliyopatika chini ya mfumo huo.

Aliyasema hayo wakati wa mahojiano maalum na kituo kimojawapo cha redio Zanzibar na kusema maridhiano hayo ya kisiasa hayakutokea kwa miujiza bali yaliasisiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Dk. Dimwa alisema Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 Ibara ya 9(a) imeahidi katika kipindi cha miaka mitano kazi kubwa itakayofanywa na CCM ni kuimarisha maridhiano, kulinda amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

Alisema kutokana na mkataba huo uliofungwa baina ya wananchi na CCM umeeleza umuhimu wa maridhiano hayo yanayotakiwa kuenziwa, kuheshimiwa na kulindwa kwa gharama yoyote.

"Wapo baadhi ya wenzetu wameanza kutoa kauli zisizofaa juu ya mfumo huu wakidai haufai, niwakumbushe kuwa haya siyo matakwa ya mtu mmoja ama kundi fulani bali ni maridhiano yalipo katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984," alifafanua Dk.Dimwa.

Alisema kazi ya kulinda maridhiano hayo imeendelea kutekelezwa vizuri na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Hussein Ali Mwinyi, kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar inakuwa miongoni mwa nchi za visiwa zilizoendelea kiuchumi.

Dk. Dimwa, alisema chini ya uongozi wake hatofumbia macho vitendo na kauli za kuingiza nchi katika machafuko na badala yake atachukua hatua kali kupitia utaratibu wa kisheria.

Alisema kama kuna viongozi na wanasiasa wasioridhika na mfumo huo waitishe mazungumzo kwa lengo la kujadili na kupata suluhu na ufumbuzi wa kudumu.

Alisema kazi nyingine ni kuwasimamia wabunge, wawakilishi na madiwani watekeleze ahadi walizotoa kwa wananchi ili kumaliza matatizo yaliyoko majimboni.

Pamoja na hayo alitaja vipaumbele vyake vitano vitakavyomwongoza katika utendaji wake kuwa ni kutekeleza majukumu yake kwa kasi yenye viwango.

Kipaumbele cha pili alisema ni kutekeleza kwa vitendo dhana ya siasa na uchumi kwa kuhakikisha anabuni miradi yenye tija itakayosaidia kujiimarisha kiuchumi.

Alisema kipaumbele cha tatu ni elimu kwa kuhakikikisha watendaji, viongozi na wanachama wanapata fursa za kusoma na kujengewa uwezo kitaaluma.

Aidha, alikitaja kipaumbele cha nne kuwa ni kuhakikisha chama kinarudi kwa wanachama wake kwa kuwasimamia watendaji na viongozi kushuka ngazi za chini, kusikiliza na kuratibu matatizo ya wananchi na kuzitafutia ufumbuzi wake.

Kipaumbele cha tano alieleza kuwa ni kuwajengea uwezo wanawake nchini ili wapate uwezo wa kugombea majimbo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

3FORM58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.41 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NEEMA MICHAEL HAULE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**BERNARD BEATUS KANIZIO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of 02, 2023

Dated at DAR ES SALAAM this 20 day of 01, 2023

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA VYETI



**JENIVA JOSEPHAT** anatangaza kupotelewa na begi lenye vyeti taaluma ikiwepo cheri cha chuo kikuu cha Dodoma cha mwaka 2021, index namba T/UDOM/2018/04367 na cheti cha kidato cha nne mwaka 2014, Kyaka Sekondari index namba s. 2162/000 pamoja na vyeti vingine kikiwamo cha taifa na cha mpigakura. Mtu yeyote atakay vipata awasiliane kwa namba **0752115167**
**RB: KAG/KAY/RB/466794/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FRANK TABURUTI KANIKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **KAZIMOTO COMPLEX (T) LIMITED** namba za usajili **MC307CJU** aina ya **TVS,** Chassis No. **MD625AFK74KIC00442,** Engine No. **AF7CK1700419.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/36546/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DIOCESE OF IRINGA** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya S**UZUKI SAMURAI** yenye namba za usajili **T 577 AGJ** LENYE **CHASSIS NAMBA: SJ51110102 ENJINI NAMBA G13A488629** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/52375/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 30/2022**

**STANSLAUS MLELWA ————————- MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

**1.AGNES HAULE**
**2.STEFAN GEU**
**3.HARD GEU**
**4.IDIFONSI NINDI** — **WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu Maombi namba nne unataarifiwa kuwa Mwombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako au wote kwa pamoja siku ya tarehe 14/02/2023 saa 2:00 asubuhi . Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 24/01/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP. 117, R.E. 2002)**

By this deed **I, AKWILINA SEVELINI PILLY** an adults, CHRISTIAN and resident of **MATALAWE-SONGEA,** do solemnly state as follows:-

1. That, I hereby absolutely renounce and abandon the use of former name **PILI AKWILINA SEVELINI AND AKWILINA ALLY PILLY** and in place thereof do assume and adopt the name of **AKWILINA SEVELINI PILLY.**
2. That, in pursuance of such change of name as aforesaid I do hereby declare that, I shall at all material times hereinafter in all records, deed and instruments in writing and in actions, proceedings and transactions and upon all occasion whatsoever use and sign the name of **AKWILINA SEVELINI PILLY** as the name in place of the former name of **PILLY AKWILINA SEVELINI AND AKWILINA ALLY PILLY.**
3. That, I further authorizes and request all people to designate and address me by such assumed name of **AKWILINA SEVELINI PILLY.**

I make this declaration consciously believing the name to be in accordance with the provisions of Oaths and statutory Act, 1966.



**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA**
**KITOU CHA MJINI MKOA WA MBEYA**
**SHAURI LA MADAI YA NDOA NO. 9/2021**

**JINALA MDAI ERICK RUBEN MWAMBEMBELA**

**JINA LA MDAIWA VENANCE JISIKAKA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

*Kanuni ya 18 ya kanunu za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo*

KWA: **VENANCE JISIKAKA**
Kwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za madai)
**NI JUU YA MAOMBI YA KUKAZIA HUKUMU**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 Mwezi 02 Mwaka 2023, saa 08:30 asubuhi na kwa mujibu wa madai hayo na kwa kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyousu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
Hati hii imetolewa kwa Amri na mhuri wa Mahakakama hii leo tarehe 03/02/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED OMARY MUNDYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC661 CSP .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MTW/MTW/RB/46215/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN BOSCO MUNG'OSI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T887DMJ** aina ya Toyota **VITZ,** Chassis No. **SCP905106206,** Engine No. **2SZ2231009.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/53292/2023.**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 31/2022**
**Asilia Shauri la jinai 41/2021, Mahakama ya Wilaya Chunya**

**JAMHURI................................MRUFAA**
**DHIDI YA**
**JUMA TANGANYIKA ....................MJIBU RUFAA**

**KWA BWANA: JUMA TANGANYIKA**
**POPOTE ULIPO..........TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 13/02/2023 siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi bila kukosa
**ELEWA KWAMBA,** ukikosa siku hiyo, shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa
Hati hii imetolewa na Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 13/12/2022

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

The Guardian
The Home of Great Newspaper

Our Regional Offices and Representatives






*Feel free to contact for:*
ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS

HEAD OFFICE
THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz | The Guardian @Theguardiantz | IPPmedia


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Marekani: Puto la China ni la kijeshi

**WASHINGTON,** Marekani

VYANZO vya kijasusi vya Marekani vimesisitiza kuwa puto lililodunguliwa Jumamosi ya wiki iliyopita lilitumiwa na Jeshi la China kwa ajili ya ujasusi.

Maofisa ambao hawakutajwa majina waliliambia gazeti la Washington Post jana kwamba wanaamini puto kama hizo zilitumika kukusanya taarifa za kijasusi kwenye maeneo yanayohusika kimkakati.

Aidha, maofisa wa China walikanusha kutumia puto hizo kwa uchunguzi, huku ofisa mmoja aliliambia gazeti la Washington Post kwamba jumuiya ya kijasusi ya Marekani inaamini kuwa baadhi ya puto hizo zilikuwa zikisafirishwa kutoka Hainan, kisiwa cha kusini mwa China ambacho kina kambi ya jeshi la wanamaji.

Taarifa ya kijasusi ya taifa hilo ilithibitisha kwamba puto hilo lilikuwa sehemu ya mpango wa uchunguzi wa angani unaoendeshwa na Jeshi la Ukombozi la watu kutoka Hainan.

Wiki iliyopita, Pentagon ilisema puto la pili la kijasusi la China limeonekana juu ya Costa Rica na Venezuela.

Hata hivyo kupatikana kwa puto zinazodaiwa kuwa za kijasusi kumesababisha mzozo wa kidiplomasia kati ya Marekani na China. **BBC**

## Tshisekedi, mazingira ya biashara DRC yameboreka

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Félix Tshisekedi, amesema mazingira ya uwekezaji katika taifa hilo yameboreka na kwamba wako tayari kutekeleza sehemu yake katika mpito wa nishati, kuwa mahali pa chaguo barani Afrika kutokana na rasilimali muhimu.



Tshisekedi (pichani) alifanya ziara nchini Afrika Kusini ili kuwashawishi wawekezaji kufikiria nchi yake, licha ya ukosefu wa usalama mashariki mwa taifa hilo.

Aidha, DRC inatajwa kuwa mzalishaji mkubwa zaidi duniani wa cobalt na kwamba ina ardhi yenye akiba ya shaba na ambayo haijatumika na lithiamu, madini muhimu kwa ajili ya utengenezaji, hasa wa betri za magari ya umeme.

Kinshasa pia inatarajia kupata ufadhili wa kuendeleza mabadiliko ya madini yake muhimu, ili kunufaika zaidi na utajiri wake, ikiwa imesalia mwaka mmoja kabla ya uchaguzi wa urais, uliopangwa kufanyika mwezi Desemba 2023. **RFI**

# Vifo vyafikia watu 8,700 tetemeko Uturuki, Syria

**ANKARA,** Uturuki

ZAIDI ya watu 8,700 wametajwa kufariki dunia nchini Uturuki na Syria kutokana na tetemeko la ardhi lililotokea mwanzoni mwa wiki, huku shirika la maafa la Uturuki likibainisha kuwa idadi ya vifo nchini humo imefikia 6,234.

Aidha, inaelezwa kuwa ni vigumu kuthibitisha idadi ya vifo nchini Syria, lakini vyombo vya habari vya serikali vilisema takribani watu 2,500 wamekufa.

Inaelezwa kuwa waokoaji wamefanya kazi usiku kucha nchini Uturuki na Syria kutafuta manusura wa tetemeko hilo na kwamba hali mbaya ya hewa na baridi kali vinafifisha matumaini ya kuwapata wengi wakiwa bado wazima.

Wafanyakazi wa vitengo vya dharura wa Uturuki na Syria wanaungwa mkono na wengine kutoka mataifa mbalimbali, huku msaada wa kimataifa ukiendelea kuwasilishwa katika mataifa hayo.

**Nchini Syria, shirika la habari la serikali SANA liliripoti kuwa watu zaidi ya 1,449 wamejeruhiwa katika maeneo yanayodhibitiwa na serikali.**

Makamu wa Rais wa Uturuki, Fuat Oktay, alisema zaidi ya watu wengine 34,810 wamejeruhiwa nchini humo, wakati shughuli za utafutaji zikiendelea.

Nchini Syria, shirika la habari la serikali SANA liliripoti kuwa watu zaidi ya 1,449 wamejeruhiwa katika maeneo yanayodhibitiwa na serikali.

Timu za waokoaji kutoka Korea Kusini, Marekani, Bosnia Herzegovina, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu zimetajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizotuma msaada kuunga mkono operesheni za kuwatafuta watu chini ya kifusi.

Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), lilisema vikundi viwili vya wataalamu wake wa uokoaji vimewasili Uturuki mapema jana.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ujerumani Nancy Faeser, alisema waokoaji takribani 40 kutoka Shirika la Misaada la Ujerumani (ISAR) walikuwa tayari nchini Uturuki, pamoja na maofisa kadhaa wa jeshi la polisi.

Inaelezwa kuwa huko Berlin, vikundi vya jamii ya Waturuki na Wakurdi viliratibu kukusanya, kupanga na kutuma michango ya misaada kutoka kwa watu wa jamii hizo wanaoishi Ujerumani na kwamba operesheni kama hizo zilikuwa zikiendelea pia Frankfurt na Munich.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa Umoja wa Mataifa (UN) umetoa dola milioni 25 kutoka mfuko wake wa dharura kwa ajili ya msaada wa kibinadamu kwa waathiriwa wa tetemeko la ardhi nchini Uturuki na Syria.

Kamishna wa Umoja wa Ulaya (EU) anayeshughulikia mizozo Janez Lenarcic, alisema timu 27 za waokoaji kutoka nchi 19 wanachama wa umoja huo zimepelekwa Uturuki kusaidia, akieleza kuwa timu hizo zinajumuisha wataalamu 1,150 na mbwa 70 wenye mafunzo ya kunusa. **BBC/DW**



Maofisa wa uokoaji wakiwa wamembeba mtoto miongoni mwa manusura waliookolewa kwenye vifusi vya nyumba zilizoporomoka baada ya kukumbwa na tetemeko la ardhi nchini Uturuki. **PICHA: DW**

# Biden, hali ya Marekani ni imara

**WASHINGTON,** Marekani

"KWASABABU nafsi ya taifa hili ina nguvu, uti wa mgongo wa taifa ni imara na wananchi wa taifa hili wana nguvu, hali ya taifa ni imara," alisema Rais wa Marekani Joe Biden.

Biden (pichani) alitoa kauli hiyo ya matumaini usiku wa kuamkia jana wakati wa hotuba yake ya pili kuhusu hali ya taifa la Marekani, akipongeza mafanikio yake ya kisheria na kisera.

Biden alihutubia bunge ambalo Spika wake Mrepublican Kevin McCarthy, aliapa kutumia wingi mdogo wa Warepublican katika baraza hilo la wawakilishi kupinga vipaumbele vingi vya Biden.



"Kupambana kwa ajili ya kupambana, kuwania madaraka kwa ajili ya madaraka, mizozo kwa ajili ya mizozo, haitufikishi popote," alisema na kuongeza;

"Huu umekuwa mtazamo wangu wa nchi yetu kila wakati na najua ni mtazamo wa wengi kati yenu, kuboresha nafsi ya taifa hili, kujenga upya uti wa mgongo wa Marekani," alisema Biden.

Aidha, Biden alizungumza kwa undani juu ya suala ambalo Wamarekani wanasisitiza ni muhimu kwao, akieleza kuwa wanajenga uchumi ambapo hakuna mtu atakayeachwa nyuma, ana kwamba ajira zimerudi kwenye viwango vya juu.

Vile vile, Biden alisema utawala wake ulibuni rekodi ya ajira mpya milioni 12 na kwamba ni ajira nyingi zaidi zilizobuniwa katika miaka miwili kuliko Rais yoyote ambaye aliwahi kubuni katika miaka minne.

Pia alitaja miongoni mwa mafanikio yake ikiwamo vita dhidi ya janga la Covid.

"Miaka miwili iliyopita Covid ilifunga biashara zetu, shule na ilitudhuru sana, leo Covid haidhibiti tena maisha yetu," alisema. **VOA**

# KASEJA AFUNGUKA UBORA WA MANULA, DIARRA BARA

**Na Hadija Mngwai**

WAKATI Bodi ya Ligi Kuu Bara (TPLB), imetoa takwimu za viwango vya magolikipa wanaoshiriki katika ligi hiyo, aliyekuwa golikipa wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, amesema Djigui Diarra wa Yanga na Aishi Manula anayedakia Simba ni walinda mlango wazuri kwa sasa hapa nchini.

Katika orodha iliyotolewa na TPLB, Diarra ndiye anayeongoza kutokana na kuwa na Clean Sheets 13 na anafuatiwa na Manula ambaye katika mechi 11, nyavu zake hazikutingishwa.

**Kaseja aliliambia gazeti hili viwango vya magolikipa hao ni vya juu na kwa kiasi kikubwa wanazisaidia timu kuvuna pointi na kufanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali.**

Kipa huyo wa zamani wa Simba, Yanga na Moro United alisema Clean Sheets za golikipa hutegemea uwezo wa timu lakini pia huchangiwa na kiwango cha juu cha mlinda mlango husika ambaye huokoa mashambulizi mbalimbali na kuonekana shujaa.

Alisema viwango walivyofikia Ashi na Diarra kwa sasa si vya kufananishwa na makipa wengine wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Clean Sheets au kuokoa inategemea na timu inayocheza, timu inaweza kusababisha upate Clean Sheets au wewe mwenyewe unaweza kusababisha. Kila mtu anajinsi anavyoangalia yeye, kwangu naona ni timu ambayo inafanya wewe upate Clean Sheets, lakini golikipa mzuri ni vile unafanya saving na kucheza hivyo mtu anaona kuna jambo zuri analifanya kufananisha na mwingine," alisema Kaseja.

Aliongeza Aishi na Diarra ni wachezaji ambao wameshajiweka katika 'levo' nyingine na hawapaswi kulinganishwa na magolikipa wachanga.

"Hao wengine wanaokuja wanafanya vizuri lakini kikubwa ni kuwapa sapoti, naamini watakuja kufanya vizuri huko mbele," Kaseja aliongeza.

Kwa sasa Kaseja ni kocha wa magokipa wa Kagera Sugar inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.




Meneja Mkuu wa Kampuni ya Betika Tanzania, Tumaini Maligana (kulia), akizungumza wakati wa uzinduzi wa msimu wa tano wa droo ya Mtoko wa Kibingwa, kushoto ni Ofisa Habari wa kampuni hiyo, Rugambwa Juvenalius. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kidunda, Tony kupimwa afya

**Na Saada Akida**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Selemani Kidunda (kulia) na Tony Rashid, wanatarajiwa kupima afya wiki ijayo tayari kwa maandalizi kuelekea katika pambano litakalofanyika Februari 24, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Kidunda atapigana na Mkongomani Patric Mukala katika pambano la kuwania mkanda wa ubingwa wa Afrika unaotambuliwa na Shirikisho la ABU huku Tony anatarajia kutetea mkanda wake wa ubingwa dhidi ya Sabelo Nganyimana kutoka Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Promota wa pambano hilo, Saadah Salum, alisema mabondia watapima uzito ifikapo Februari 18, mwaka huu ikiwa ni utaratibu wa kawaida kabla ya kupanda ulingoni.

"Ukiangalia rekodi ya Kidunda na Tony, hata ukirejea kwa wapinzani wao ambao watacheza nao unaona namna pambano litakavyokuwa kubwa na lenye ubora, kila mmoja anahitaji kuonyesha kiwango kizuri na kupata mkanda huo," alisema Saadah.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki wa mchezo huo kujiandaa kuona burudani nzuri kutokana na kila bondia amejipanga kulinda heshima yake pamoja na bendera ya nchi.

Aliwataja mabondia wengine watakaopima afya siku hiyo ni pamoja na Emmanuel Mwakyembe atakayepigana na Francis Miyeyusho, Mbaraka Mtange dhidi ya Hamza Mchanjo, Mwinyi Mzengela vs Ajemi Amani, Abdul Kubila vs Msabaha Salum, Omary Baraka vs Mukhsin Kizota, Ahmady Pelembela vs Idd Pazzi na Florah Malechela atakayepigana na Halima Bandola, ikiwa ndio pambano pekee la wanawake.



# Baobab yaihofia Simba Queens Dar

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajia kuendelea kwa mabingwa watetezi, Simba Queens kuwakaribisha Baobab Queens katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Baobab Queens kutoka Dodoma, Juma Maulid, aliliambia gazeti hili timu yake itaingia katika mchezo huo kwa tahadhari kutokana na ubora wa wapinzani wao.

Maulid alisema wanaiheshimu Simba Queens kutokana na ubora wa wachezaji wake na uzoefu waliokuwa nao baada ya mechi mbalimbali za ndani na kimataifa.

"Tunaiheshimu Simba kwa sababu ni miongoni mwa timu bora kwa upande wa Ligi Kuu ya Wanawake, ina wachezaji wazuri wa ndani na wale wa kigeni, hatutawadharau," alisema Maulid.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wote wanaendelea vyema na kuongeza hakuna nyota ambaye atakaukosa mchezo huo.

"Wachezaji wote wapo vizuri kisaikolojia kuelekea kwenye mchezo huo, wenye watarajie kupata upinzani mkubwa kwa sababu tumewasoma," aliongeza kocha huyo.

# Hat-trick ya tatu Ligi ya Wanawake

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Mnigeria, Nkor Blessing, amefunga mabao matatu katika mechi iliyomalizika kwa timu yake ya Yanga Princess kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya The Tiger Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Hiyo inakuwa ni 'hat-trick' ya tatu kwenye Ligi Kuu ya Wanawake, mbili zikiwa ni za wachezaji wa Simba Queens, Opa Clement ambaye ni Mtanzania na Mkenya, Jentrix Shikangwa.

Nkor, alifunga mabao hayo matatu, huku mengine yakipachikwa na Mnigeria mwenzake, Chioma Wogu na Nadege Atanhloueto kutoka Benin.

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya nane ya Ligi Kuu ya Wanawake ambapo baada ya ushindi huo, Yanga Princess imefikisha pointi 17 sawa na JKT Queens ambayo jana jioni iliwaalika Fountain Gate Princess huku leo mabingwa watetezi, Simba Queens watawavaa Baobab Queens kwenye Uwanja wa Uhuru.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Sebastian Nkoma, alisema ligi hiyo imekuwa na ushindani mkubwa lakini jambo muhimu kwao ilikuwa ni kupata pointi tatu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA KANE

MANCHESTER United inapanga kutoa pauni milioni 100 kumnunua nahodha wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, 29 au mchezaji wa kimataifa wa Napoli (24), Victor Osimhen. ***(Telegraph)***

### WAARABU KUINUNUA UNITED

WAWEKEZAJI kutoka nchini Qatar wanatarajia kuwasilisha rasmi ofa ya kuinunua Manchester United katika siku za hivi karibuni baada ya familia ya Glazer inayoimiliki klabu hiyo kutangaza kuiuza. ***(Mail)***

### CITY SASA NJIA PANDA

MANCHESTER City inataka kuzipiku Real Madrid na Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 19, kutoka Borussia Dortmund katika dirisha la usajili la majira ya joto, lakini tishio la kuwekewa vikwazo baada ya kushtakiwa na Ligi Kuu England linaweza kuwazuia kufanya hivyo. ***(Telegraph)***

### KUMBAKIZA BELLINGHAM

KLABU ya Borussia Dortmund inaandaa ofa maalumu ili kumshawishi nyota wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham kusalia katika klabu hiyo ya Ujerumani kwa msimu mwingine. ***(90MIN)***

### ARSENAL KUMUUZA BALOGUN

ARSENAL bado inaweza kuamua kumuuza mchezaji wa kimataifa wa England, Folarin Balogun, 21, katika msimu wa joto, licha ya mshambuliaji huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia akicheza kwa mkopo kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, akiwa na Reims msimu huu. ***(Sun)***

### IRAOLA ANUKIA LEEDS

KOCHA wa Rayo Vallecano, Andoni Iraola, anafahamika kuwa miongoni mwa wanaowania kuchukua nafasi ya Jesse Marsch kama kocha mpya wa Leeds United. ***(Independent)***

### LEEDS YAMKATAA MAURICIO

KLABU ya Leeds United haitamteua aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Marcelo Bielsa au kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino. ***(Star)***

### INTER ILIMTAKA MESSI

INTER Milan ilifanya mazungumzo na nahodha na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, 35, kabla ya nyota huyo wa zamani wa Barcelona kuamua kujiunga na Paris St-Germain. ***(Goal)***


### ZANIOLO KUTUA GALATASARAY

WINGA wa AS Roma ya Italia, Nicolo Zaniolo, 23, amesafiri hadi jijini Istanbul nchini Uturuki kukamilisha uhamisho wa kujiunga na Galatasaray. ***(Mail)***

### BUSQUETS ATAKIWA ARABUNI

KIUNGO wa kati wa Hispania, Sergio Busquets, 34, amepewa ofa ya mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 16 kwa msimu na klabu ya Saudi Arabia, Al Nassr lakini atasubiri kuona kama Barcelona itampa mkataba mpya kabla ya kufanya uamuzi. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO [illegible]KA MAGAZETI [illegible]YA




# SHERINGHMAN: CASEMIRO NI KEANE MPYA UNITED

**MANCHESTER,** England

**●●● Nyota huyo asema kiungo huyo anaitendea haki nafasi ya kiungo ambayo...**

TEDDY Sheringham amemfananisha Casemiro na mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, akidai Mbrazil huyo ndiye jenerali wa kiungo ambaye klabu hiyo ilikuwa imemkosa kwa muda mrefu na sasa wamempata.

Casemiro amekuwa akisifiwa tangu uhamisho wake wa paundi milioni 70 kutoka Real Madrid katika msimu wa joto, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akiwa na mchango mkubwa katika kuimarika kwa Mashetani Wekundu hao msimu huu chini ya kocha, Erik ten Hag.

United italazimika kuvumilia kidogo kucheza bila Casemiro kwenye mechi tatu zijazo za Ligi Kuu England, baada ya Mbrazil huyo kuonyeshwa kadi nyekundu ya kwanza katika maisha yake ya soka akiwa na United, dhidi ya Crystal Palace Jumamosi iliyopita.

**Sheringham alisema kiungo huyo anaweza kufananishwa na Keane, ambaye alionyesha viwango vyake kama nahodha wa Manchester United pale Old Trafford.**

Sheringham alishinda mataji matatu ya Ligi Kuu England akiwa na United inayoongozwa na Keane, ikiwa ni pamoja na kucheza nafasi muhimu na kutwaa mataji katika msimu wa 1998-99 likiwamo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nitasema tu kuhusu Casemiro nadhani ni kama Roy Keane ambaye wamemkosa kwa miaka nane iliyopita," alisema Sheringham, ambaye alifunga mabao 46 katika mechi 153 za United.

"Jenerali huyo wa kiungo ambaye ana molari na uelewa wa mchezo wa kati afanye nini ili kuhakikisha timu yake inafanya vizuri kadri ya uwezo wao.

"Hana wasiwasi tu juu yake mwenyewe, ninampenda. Labda alifikiri alipaswa kutekeleza jambo fulani wakati huo (wa kadi yake nyekundu)".

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,074,7

MECHI KALI

AL WAHDA
VERSUS
AL NASR RIYADH

1 | 5.76
X | 4.16
2 | 1.52

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BUSQUETS AIPA PIGO BARCELONA




**BARCELONA,** Hispania

NAHODHA wa Barcelona, Sergio Busquets yuko shakani kuivaa Manchester United wiki ijayo baada ya vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kuthibitisha aliteguka kifundo cha mguu kwenye mchezo dhidi ya Sevilla.

Busquets alijeruhiwa katika ushindi wa mabao 3-0 wa Barca kwenye LaLiga Uwanja wa Camp Nou Jumapili baada ya kuchezewa vibaya na Youssef En-Nesyri na kutolewa nje muda mfupi baadaye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye amecheza mechi 27 kati ya 31 za Barcelona msimu huu, alifanyiwa uchunguzi Jumatatu na kubaini ameumia kwenye kifundo cha mguu wake wa kushoto.

Ingawa hakuna ratiba rasmi ya kurudi kwa Busquets, mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania ameripotiwa atakuwa nje ya uwanja kwa angalau wiki mbili.

Hiyo itamfanya Busquets kutoshiriki katika mechi za LaLiga dhidi ya Villarreal na Cadiz, na mchezo wa kwanza wa raundi ya mtoano wa Ligi ya Europa dhidi ya United utakaochezwa Februari 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Old Trafford.



## Argentina, Uruguay, Paraguay kuandaa Kombe la Dunia 2030

**BUENOS AIRES,** Argentina

MABINGWA wa Kombe la Dunia, Argentina wamethibitisha rasmi kuungana na Uruguay, Paraguay na Chile kuomba kuandaa fainali za michuano hiyo zitakazofanyika mwaka 2030.

Awali Argentina na Uruguay ndio waliamua kuungana kuandaa michuano hiyo tangu mwaka 2017, lakini sasa zimeongezeka nchi nyingine mbili. Uruguay ilikuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia la kwanza mwaka 1930.

Akizungumza baada ya kuthibitishwa kwa ofa hiyo ya nchi nne, Rais wa Shirikisho la Soka la Argentina, Claudio Tapia, aliweka wazi matumaini yake ya kurejesha michuano hiyo barani huko ambako ilifanyika kwa mara ya kwanza.

"Tuna uwezekano wa kuandaa Kombe hili la Dunia," alisema. "Ina historia, kiini, shauku ambayo sisi Waamerika Kusini tunaishi soka. "Leo ni siku muhimu sana kwa historia ya nchi hizi nne, kati mashirikisho haya man ambayo zamani yalian kwa ndoto.

"Tunajua hii ni dham kubwa sana na lazi tuonyeshe ulimwen Argentina, Uruguay, Par guay na Chile ziko tay kuandaa Kombe la Dun la 2030."

Rais wa Shirikisho soka la Amerika Kus (CONMEBOL), Alejand Dominguez, aliunga mk no maoni hayo na kuo geza: "Leo tuna timu, tunaamini katika ukuu.

741,067/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/02/23 | 18:00 | Southampton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 02. 11/02/23 | 18:00 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 11/02/23 | 18:15 | UD Almeria vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 04. 11/02/23 | 22:45 | Lazio Rome vs Atalanta BC | 2.27 | 3.35 | 3.00 |
| 05. 11/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 06. 12/02/23 | 09:00 | Macarthur FC vs Wellington Phoenix FC | 2.55 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 12/02/23 | 15:00 | Toulouse FC vs Stade Rennes | 3.05 | 3.35 | 2.25 |
| 08. 12/02/23 | 16:00 | Getafe CF vs Rayo Vallecano | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 09. 12/02/23 | 16:30 | Vitesse Arnhem vs FC Utrecht | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 12/02/23 | 17:00 | Angers SCO vs AJ Auxerre | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 12/02/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs Stade Brest 29 | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 12/02/23 | 17:30 | Hertha BSC vs Borussia Monchengladbach | 2.75 | 3.50 | 2.37 |
| 13. 12/02/23 | 18:15 | RC Celta de Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.05 | 2.24 |
| 14. 12/02/23 | 19:30 | 1. FC Cologne vs Eintracht Frankfurt | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 15. 12/02/23 | 20:30 | Real Valladolid vs CA Osasuna | 2.60 | 3.05 | 2.80 |
| 16. 12/02/23 | 21:00 | Sporting Lisbon vs FC Porto | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 17. 12/02/23 | 22:45 | Olympique Lyon vs RC Lens | 2.39 | 3.40 | 2.80 |

MECHI ZA USHINDI
“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE
“2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 09/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1574 | Hong Linh HA Tinh FC vs CLB Viettel | 3.51 | 2.89 | 2.13 |
| 14:00 | 4714 | Gokulam Kerala FC vs Minerva FC | 2.70 | 3.01 | 2.52 |
| 15:15 | 2125 | TT Ha Noi vs Cong Anh Nhan Dan | 1.89 | 3.05 | 3.50 |
| 15:45 | 3395 | El Ittihad Alexandria vs Aswan | 1.98 | 3.18 | 3.93 |
| 16:00 | 2251 | AL Baten vs Al Shabab Riyadh | 5.98 | 4.38 | 1.48 |
| 16:00 | 4987 | Busoga United vs Maroons FC | 2.33 | 2.80 | 2.80 |
| 16:00 | 5052 | Wakiso Giants FC vs Kampala City Council | 2.90 | 2.90 | 2.20 |
| 16:10 | 3648 | Al Oruba vs Al Nahda (Oman) | 4.77 | 3.27 | 1.71 |
| 16:40 | 4460 | AL Nasr vs Kazma SC | 3.89 | 3.42 | 1.82 |
| 17:00 | 2610 | Jamshedpur vs ATK Mohun Bagan | 3.06 | 3.31 | 2.12 |
| 17:00 | 3562 | Aalesunds vs Brann | 2.41 | 3.83 | 2.35 |
| 18:00 | 1800 | Al Taawon vs Al Fateh (KSA) | 1.88 | 3.20 | 3.40 |
| 18:00 | 2430 | Queretaro U20 vs Leon U20 | 2.56 | 3.47 | 2.37 |
| 18:00 | 3177 | Atlas U20 vs Monterrey U20 | 1.91 | 3.42 | 3.53 |
| 18:30 | 1409 | Najma Manama vs ISA Town | 1.52 | 4.14 | 4.97 |
| 18:30 | 2890 | Malkiya Club vs Etehad Alreef | 1.49 | 3.99 | 5.59 |
| 18:30 | 4880 | AL Ittihad Bhr vs Qalali | 2.04 | 3.26 | 3.31 |
| 19:10 | 1900 | AL Qadsia vs Al Jahra | 1.49 | 3.75 | 4.90 |
| 19:15 | 2342 | Al Shabab (Oman) vs Al Seeb | 5.80 | 3.63 | 1.53 |
| 19:30 | 2762 | Lamia vs PAOK | 5.07 | 3.52 | 1.62 |
| 20:00 | 2287 | Apollon Limassol vs Karmiotissa | 1.46 | 4.27 | 6.61 |
| 20:00 | 3314 | Nea Salamis vs Anorthosis Famagusta | 2.82 | 3.09 | 2.55 |
| 20:30 | 1062 | Casa Pia Atletico vs Nacional Madeira | 1.51 | 3.84 | 5.60 |
| 20:30 | 1385 | Al Wehda vs Al Nasr Riyadh | 5.76 | 4.16 | 1.52 |
| 20:45 | 2975 | Twente vs Ajax | 3.26 | 3.47 | 1.98 |
| 21:00 | 2593 | St Lucia vs Marsaxlokk FC | 3.74 | 3.43 | 1.85 |
| 21:00 | 4832 | Puskas Akademia vs Ujpest FC | 2.05 | 3.32 | 3.21 |
| 21:00 | 5098 | GD Estoril vs Boavista | 2.44 | 3.14 | 2.89 |
| 21:30 | 3781 | Floresta CE vs Pague Menos CE | 2.09 | 2.90 | 3.62 |
| 21:30 | 4056 | AEK Athens vs Olympiakos | 1.93 | 3.22 | 3.69 |
| 21:30 | 4596 | Alecrim RN vs Globo RN | 2.44 | 3.31 | 2.58 |
| 22:00 | 2166 | Gzira United vs Qala St Joseph FC | 1.11 | 7.28 | 15.60 |
| 22:00 | 4503 | Fram Reykjavik vs Grotta | 1.39 | 5.38 | 5.18 |
| 23:00 | 1104 | Lorient vs Lens | 3.54 | 3.49 | 1.98 |
| 23:00 | 1604 | ADO Den Haag vs GO Ahead Eagles | 3.32 | 3.47 | 1.96 |
| 23:00 | 3295 | Ecuador U20 vs Venezuela U20 | 1.79 | 3.32 | 4.15 |
| 23:30 | 3221 | Sporting Braga vs Benfica | 3.38 | 3.43 | 1.95 |

IJUMAA - 10/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1344 | Santo Andre SP vs EC Agua Santa SP | 2.16 | 2.95 | 3.36 |
| 00:00 | 3331 | Real Cartagena vs Patriotas FC | 3.88 | 3.37 | 1.83 |
| 00:00 | 3809 | Sebaco FC vs Indigenas de Matagalpa FC | 1.62 | 3.50 | 4.20 |
| 01:00 | 1698 | Maranhao MA vs Iape MA | 1.65 | 3.58 | 4.67 |
| 01:00 | 2240 | Avenida RS vs Aimore RS | 2.14 | 2.80 | 3.62 |
| 01:00 | 5360 | SE Queimadense PB vs Souza PB | 4.55 | 3.11 | 1.79 |
| 01:30 | 3137 | Uruguay U20 vs Paraguay U20 | 1.82 | 3.32 | 3.99 |
| 01:30 | 4331 | Palmeiras vs Inter De Limeira SP | 1.28 | 4.66 | 9.33 |
| 03:00 | 2905 | Audax Italiano vs Union Espanola | 2.05 | 3.26 | 3.26 |
| 03:00 | 3478 | Atletico Catarinense SC vs Joinville | 2.65 | 2.55 | 2.65 |
| 03:00 | 3882 | CA Boston River vs Zamora FC | 1.65 | 3.45 | 4.86 |
| 04:00 | 4190 | Colombia U20 vs Brazil U20 | 3.22 | 3.38 | 2.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SINGIDA BS FC YATAJWA KUMWINDA KAKOLANYA

**Na Saada Akida**

AKIWA amebakiza miezi sita katika mkataba wake, golikipa chaguo la pili wa Wekundu wa Msimbazi, Beno Kakolanya (pichani), anadaiwa kuivutia Singida Big Stars inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Pia inadaiwa kuna klabu moja kutoka Saudi Arabia imeweka mezani ofa ya kuanzia Dola za Marekani 100,000 hadi 150,000 kwa ajili ya kupata saini ya Kakolanya ambaye amekuwa na kiwango kizuri kila anapopata nafasi ya kucheza.

Singida Big Stars inahitaji kupata golikipa mpya baada ya aliyekuwa mlinda mlango wake namba moja, Metacha Mnata kujiunga na Yanga katika dirisha dogo la usajili.

**Meneja wa Kakolanya, Suleiman Haroub, alisema jana jijini Dar es Salaam bado hajapokea ofa kutoka katika timu yoyote ya hapa nchini ambayo imeweka wazi inahitaji huduma ya nyota huyo.**

Haroub alisema endapo atapokea ofa ya klabu yoyote, watafanya mazungumzo na hatimaye watafikia uamuzi kwa faida ya mchezaji husika lakini wataipa kwanza nafasi Simba.

Aliongeza anaimani kubwa na Simba kuhitaji kuendelea kupata huduma ya kipa huyo kwa sababu tayari wameanza hatua za awali za mazungumzo ya kumwongezea mkataba mpya.

“Hadi sasa ni Simba pekee ambao wanahitaji kumwongezea mkataba mwingine wa kusalia ndani ya kikosi cha timu yao,” alisema meneja huyo.

Kakolanya ndiye golikipa aliyesimama langoni katika mechi zote za mashindano ya Kombe la FA ambayo yamefika kwenye hatua ya 32 bora.

## Yanga yawatisha wenyeji Montasir

INATOKA UKURASA 24

wameziona, kwa hiyo wembe utakaotumia ni ule ule,” alisema Kamwe.


Naye Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kwa kiwango walichonacho sasa wachezaji wa timu hiyo, wanaamini watapata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya kwanza.

“Tutapambana kwa ajili ya wanachama, mashabiki wa Yanga na Watanzania kwa ujumla, uzuri tunaenda kwenye uwanja ule ule, tunaamini kitatokea kizuri zaidi ya kile cha mwanzo, katika mechi hizi ukipata ushindi mechi ya kwanza au sare ugenini, ni kitu kizuri ili kufikia malengo,” alisema meneja huyo.

Dickson Job, aliliambia gazeti hili yeye na wachezaji wenzake wa Yanga wapo tayari kwa asilimia zote kuipambania timu pamoja na taifa.

“Bahati nzuri tumekuja mahali ambapo tulishafika, tunataka tukirudi nyumbani tupigiwe makofi kwa mara nyingine tena,” alisema beki huyo wa kati.

Yanga ilicheza dhidi ya Club Africain nchini humo Novemba 9, mwaka jana na ikapata ushindi bao 1-0 na kufanikiwa kutinga hatua hiyo, baada ya mechi ya kwanza ya nyumbani Novemba 2, kumalizika kwa suluhu.




## Simba: Tutawafurahisha

INATOKA UKURASA 24


cha wachezaji kamili akiwamo kiungo wetu, Jonas Mkude ambaye kwa sasa yuko fiti, anaendelea vizuri na maandalizi ya mchezo huo wa Jumamosi,” alisema kiongozi huyo.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya CAF ni Yanga ambayo yenyewe itakuwa ugenini Tunisia kwa ajili ya kuwavaa US Montastir kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Alhamisi Februari 9, 2023

Nipashe

'Casemiro ni Keane mpya wa United' UKURASA 21

# Simba: Tutawafurahisha

## ●●● Kikosi kimeondoka nchini leo na matumaini huku jezi mpya...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kinaondoka nchini leo kuelekea Guinea kuwafuata Horoya kwa ajili ya mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema wataanza vyema hatua ya makundi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

**Horoya AC itaikaribisha Simba katika mechi ya kwanza itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Nongo-Stade General Lansana Conte ulioko katika mji wa Conakry nchini humo.**

Robertinho alisema kupata ushindi katika mechi ya kwanza na ya ugenini itakisaidia kikosi chake kujiamini kabla ya kurejea nyumbani kwa ajili ya kuikaribisha Raja Casablanca kutoka Morocco.

"Tuko tayari kwa mapambano, tunakwenda kutafuta matokeo mazuri, tumejiandaa vizuri na tunaamini pia wapinzani wetu, wenyeji wa mechi hiyo nao wamejipanga, lakini ninaamini wachezaji wangu watatupa matokeo mazuri," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema wachezaji wake watashuka uwanjani kwa ajili ya kusaka heshima ya klabu kwa sababu wanafahamu hakuna mechi rahisi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara au katika mashindano ya Afrika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema klabu hiyo inaipongeza Kampuni ya M-Bet kwa kukubali kutumia nembo tofauti na masharti yaliyoko kwenye mkataba wao wa udhamini.

Kajula alisema hayo katika uzinduzi wa jezi zitakazotumiwa rasmi na timu yao kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kuongeza hatua hiyo ni ya kizalendo na inaleta tija kwa nchi hasa ukizingatia Tanzania ni nchi ya nne kwa kuwa na vivutio bora vya utalii duniani.

"Simba itahamasisha ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuutangaza utalii kupitia mashindano haya. Sisi ni wazalendo wa kweli," alisema Kajula.

Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema kampuni yao haina kipingamizi kwa timu hiyo kutumia nembo ya Visit Tanzania kwa sababu itatumika kutangaza utalii wa nchi.

"Kampuni ya M-Bet ni wazalendo, baada ya kupokea ombi la Simba hatukuwa na kipingamizi, kupitia mashindano ya Ligi ya Mabingwa, Simba inakwenda kutangaza vivutio vya utalii na hivyo kuongeza pato la taifa," alisema Mushi.

Aliongeza kila hatua ambayo watavuka, basi Tanzania itaendelea kutangazwa na matunda yake tayari yameanza kuonekana kutokana na mafanikio yaliyopatikana msimu uliopita.

Mwakilishi wa Wizara ya Utalii na Maliasili na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Bernard Mtatiro, alisema kupitia mashindano ya CAF, Simba itakuwa inaitangaza nchi.

"Tunaamini Simba SC ikitangaza utalii wa nchi, itatangaza nchi kwa ujumla kimataifa, hivyo itasaidia nchi kupata mapato zaidi kutokana na utalii, hata sekta ya ajira itaimarika, kupitia utalii zaidi ya watu milioni 1.3 hupata ajira," alisema Mtatiro.

Wakati huo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kampuni mbalimbali zilijitokeza kuwapa udhamini kwa ajili ya michuano hiyo ya kimataifa lakini hawakukubali kwa sababu ya kuwaheshimu wadhamini wao wakuu.

"Kwa kuwa tumeona faida ya kuvaa Visit Tanzania, basi tumeheshimu matakwa ya mdhamini wetu na tutaenda nao kwa miaka mitano yote, kuhusu jezi tumepanga kuanza kuuza ifikapo Februari 15, mwaka huu kwa sababu tutakuwa na jambo letu Februari 18, dhidi ya Raja Casablanca kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, " alisema Ahmed.

Aliongeza wachezaji wako katika hali nzuri wataelekea Guinea kufanya kazi ambayo itawafurahisha mashabiki na wanachama wa Simba.

"Tunatarajia kuondoka na kikosi

INAENDELEA UKURASA 23



Beki wa kati wa Simba, Henock Inonga. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga yawatisha wenyeji Montasir

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutua salama Tunisia kwa ajili ya mechi ya kwanza ya hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga imetamba kutumia 'ramani' ile ile iliyowapeleka katika hatua hiyo kutokana na kuwaondoa Club Africain, imeelezwa.

Wenyeji US Montastir itawaalika Yanga kwenye Uwanja wa Olypmique Hamadi Agrebi Redes ulioko katika jiji la Tunis Jumapili, huku uongozi ukisema wembe uliotumika kuinyoa Club Africain, ndio watautumia tena.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe (pichani), alisema kila kitu kuelekea mchezo huo kinakwenda vizuri na wanajua wanachokifanya kwa sababu wamejipanga kupata matokeo mazuri.



Kamwe alisema tayari benchi la ufundi limeshawasoma wapinzani wao na kufahamu mahali ambapo kuna makali na madhaifu.

"Wachezaji walioshinda mechi dhidi ya Club Africain ndiyo kwa asilimia kubwa tuliokuwa nao huku, na benchi la ufundi ni lile lile, asitokee tena mtu akajifanya anajua zaidi kutupa ushauri, tulishindaje Tunisia au tunahitaji kufanya nini. Sisi wanachama, mashabiki, viongozi, benchi la ufundi na wachezaji wetu ndio tunajua nini tulifanya tukashinda. Tumeona baadhi ya mechi zao na wachezaji wetu

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042